SUPA JACKPOT
TZS. 1,109,975,029
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



**Waziri** auawa kwa kupigwa risasi na mlinzi wake kisa ujira

UKURASA 3

## YALIYOMO

UKURASA WA 3



### BABU ADAIWA KUUA WAJUKUU KWA MCHI

JESHI la Polisi mkoani Songwe, linamshikilia Aloyce Nyabwanzo (51), mkazi wa Kijiji cha...

UKURASA WA 7

### WABUNIFU 700 NCHINI WAOMBA MTAJI CRDB

UKIWA umepita mwezi mmoja wa kuwatambua wabunifu wanaotaka kuendeleza miradi yao, Benki ya...

UKURASA WA 17

### KANISA LATOA VIFAA MATIBABU HOSPITALINI

KANISA la The Word of Reconciliation Ministries (WRM) limeitumia Siku ya Wafanyakazi Duniani 'Mei Mosi'...

Jumatano Mei 3, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581299

www.ippmedia.com

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US

# MAPINDUZI YA MIFUGO, UVUVI

• **Serikali** ina orodha ya mikakati 25 kuinua sekta... *Endelea ukurasa 2*



**Pikipiki 1,200 kugawiwa wataalamu kila kona**



**Migogoro ya wakulima, wafugaji yapatiwa dawa**




**Inaundwa mamlaka kusimamia uvuvi nchini**



**Wafugaji waandaliwa majani kuwatajirisha**



**Wavuvi wapatiwa boti za kisasa kuwainua**



**Mikopo maalum inayowalenga vijana**



Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo, kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

RIPOTI YA UCHUNGUZI

## Reli inayokatiza hifadhini janga kwa wanyamapori

UKURASA 4



## Imeanikwa rasmi waumini kanisa Kenya walinyongwa

UKURASA 2

**MICHEZO** ROBERTINHO AAHIDI FURAHA SIMBA LEO UK.24 **KATUNI** UK.6

# Mapinduzi ya Mifugo, Uvuvi

**Na Gwamaka Alipipi,**
DODOMA

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, amewasilisha bungeni makadirio ya mapato na matumizi ya wizara yake kwa mwaka ujao wa fedha, akitaja hatua kadhaa zenye lengo la kuleta mapinduzi ili iwe na mchango zaidi kwenye Pato la Taifa na kupambana na umaskini kwa wafugaji na wavuvi.

Ulenga ametaja mikakati 25 iliyopangwa na wizara hiyo itakayowakomboa wafugaji na wavuvi, na kuliwezesha taifa kupiga hatua kiuchumi. Ameliomba Bunge kuidhinisha Sh. bilioni 295.9 ili kutimiza malengo hayo.

Akiwasilisha jana makadirio bungeni jijini hapo, Waziri Ulega alitaja hatua kadhaa zikiwamo za kuongeza ukubwa wa soko la nyama na samaki ndani na nje ya nchi, ufugaji wa kisasa wenye faida zaidi kwa wafugaji, kuongeza malisho ya wanyama na samaki na kuongeza usimamizi wa sekta ya uvuvi kwa lengo la kuongeza mchango wa wizara yake kwenye Pato la Taifa na kupunguza umaskini nchini.

“Kwa sasa, mchango wa sekta ya mifugo kwenye Pato la Taifa ni takribani asilimia saba na sekta ya uvuvi ni asilimia 1.8. Kwa ujumla, wizara inachangia asilimia 8.8 ya pato letu na kwa hatua hizi tunazokwenda kuchukua kupitia bajeti hii, tunaamini mchango utakuwa mkubwa zaidi,” alisema Ulega.

Tofauti na miaka ya nyuma, makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo mwaka ujao wa fedha, yalionekana kuwagusa wabunge.

Ni makadirio ya kwanza ya mwaka wa fedha kwa wizara hiyo chini ya Ulega akiwa waziri kamili tangu alipoteuliwa na Rais Samia Suluhu Hassan mnamo Februari mwaka huu.

Katika hotuba yake hiyo, Ulega ambaye pia ni Mbunge wa Mkuranga, aliliomba Bunge kuidhinisha Sh. bilioni 295.9. Kati yake, Sh. bilioni 112 zitatumika kwenye sekta ya mifugo huku Sh. bilioni 183 zikienda sekta ya uvuvi.

Waziri huyo kijana alitumia hotuba yake kupongeza jitihada binafsi zilizofanywa na Rais Samia kwenye kufungua soko la biashara ya nyama katika nchi za Kiarabu - ambako alisema biashara ya nyama imeongezeka kwa takribani asilimia 46 ndani ya miaka miwili ya kwanza ya uongozi wa serikali ya awamu ya sita.

“Tanzania haikushiriki Kombe la Dunia mwaka jana nchini Qatar kwa maana ya kucheza lakini kutokana na diplomasia ya uchumi ya Mheshimiwa Rais, Tanzania ilifanya biashara kubwa ya nyama wakati huo kuliko wakati mwingine wowote kwenye historia yetu.

“Sasa tunaambiwa hata tukiuza ng'ombe wetu wote waliopo hapa Tanzania, bado hatutaweza kukidhi kiu ya wateja wa nyama yetu huko uarabuni. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kutufungulia njia,” alisema Ulega.

Kulinganisha na makadirio yaliyopita ya wizara hiyo, safari hii yamejikita zaidi katika masuala yatakayoongeza tija kwenye mifugo na uvuvi na kujielekeza katika kuifanya wizara kuwa na mwelekeo wa kibiashara na unaotaka faida ya kuwa na mifugo mingi na samaki wengi ionekane.

Ulega aliliambia Bunge kwamba wizara yake itafanya uwekezaji mkubwa katika eneo la ukuzaji wa majani kwa ajili ya ng'ombe, lengo likiwa kuhakikisha mifugo inakuwa na chakula cha uhakika na nchi iuze nje kwa kuwa zipo nchi zina shida ya majani.

“Kuna ofa tayari kutoka kwa wenzetu wa Saudi Arabia wanaotaka kununua aina fulani ya majani ya mifugo kutoka kwetu. Kama mambo yatakwenda vizuri, watu wetu watalima hapa na kupata soko la uhakika. Muda si mrefu, majani yanakwenda kuwa biashara nzuri ya kutuingizia fedha za kigeni hapa kwetu,” alisema Ulega.

Akizungumza kwa kujiamini na kuonyesha uelewa mkubwa wa masuala ya wizara yake, Ulega alisema suala la kuwa na malisho ya kutosha kwa wanyama litapunguza migogoro ya mara kwa mara baina ya wakulima na wafugaji; akisema chanzo chake kikubwa huwa ni ukosefu wa malisho.

Ulega alitumia sehemu kubwa ya hotuba yake ya jana kufafanua kwa kina kusudio la wizara yake kuanzishwa chombo cha usimamizi wa sekta ya uvuvi; akisema kwa hali ilivyo sasa, mfumo hausaidii sana usimamizi wa sekta hiyo.

“Nchi yetu ina maziwa, mito na bahari na kote huko uvuvi unafanyika. Wizara ina watu wanaosimamia eneo hilo lakini ninadhani tunahitaji kuwa na chombo - kama ilivyo kwa EWURA kwenye mafuta, ambacho watu wake watakuwa wakilala na kuamka wanaangalia masuala ya samaki tu. Samaki ni rasilimali muhimu sana na ni muhimu kuipa umuhimu inaostahili,” alisema.

Waziri huyo alilitangazia Bunge jana kwamba serikali itaendelea na mipango iliyoanza kwenye bajeti za nyuma ikiwamo kununua boti kwa ajili ya kusaidia uvuvi kwenye maji ya kina kirefu, kutoa mikopo kwa wavuvi ili kuwawezesha kununua vifaa vya kisasa vya uvuvi na kuanza ujenzi wa bandari ya uvuvi huko Kilwa.



Ulega alisema mpango wa Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi (sekta ya mifugo) kwa mwaka 2023/2024 utazingatia kuimarisha upatikanaji wa mbegu bora za mifugo.

Alisema wizara itajielekeza katika kuimarisha upatikanaji wa malisho, vyakula vya mifugo na maji kwa ajili ya mifugo, kuimarisha afya ya mifugo pamoja na kuboresha huduma za ugani.

Ulega alisema pia wataanzisha na kuendeleza vituo atamizi vya uwekezaji vya vijana, kuimarisha huduma za utafiti na mafunzo ya taaluma za mifugo.

Alisema watawezesha uongezaji thamani na biashara ya mifugo na mazao yake, kuimarisha Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) na kuanzisha skimu za umwagiliaji katika mashamba ya malisho ya Vikuge na Langwira, pamoja na ranchi za NARCO za Kongwa na Mzeri.

Alisema pia watajenga mabwawa na visima kwa ajili ya mifugo na kuanzisha mashamba darasa 150 katika mamlaka za serikali za mitaa na taasisi za wizara.

Ulega alisema wataanzisha vituo vipya vya uwekezaji vya vijana na kuendeleza vituo vingine vilivyoanzishwa, kuhimilisha ng'ombe 100,000 na kuendelea kununua madume bora na kuyagawa kwenye vikundi vya wafugaji.

Ulega alisema wataendesha kampeni ya udhibiti magonjwa kwa kujenga majosho 246, kununua dawa za kuogesha mifugo lita 56,000 na kusambaza chanjo.

Pia alisema watanunua pikipiki 1,200, magari matatu, zana za huduma za veterinari 1,100, zana za uhimilishaji 184 na kuanzisha kampasi mpya ya LITA Songwe.

Kuhusu sekta ya uvuvi, Ulega alisema watatekeleza vipaumbele vinavyoendana na kufungamanisha uchumi wa buluu hususani matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi, ikiwamo uvuvi wa asili na ukuzaji viumbe maji.

Alisema watakwenda kuimarisha uwezo wa uvuvi katika bahari kuu pamoja na kuimarisha taasisi za uvuvi ili kuongeza ushiriki katika uchumi wa buluu.

Ulega alisema wataimarisha ulinzi na usimamizi wa rasilimali za uvuvi, kuongeza uwekezaji katika miundombinu ya uvuvi na ukuzaji viumbe maji, kuimarisha uthibiti wa ubora wa mazao ya uvuvi na masoko pamoja na kuimarisha huduma za ugani wa uvuvi na ukuzaji viumbe maji.

Ulega alisema: “Tutaendelea na ujenzi wa Bandari ya Uvuvi Kilwa Masoko - Lindi, ununuzi wa meli tatu za uvuvi wa bahari kuu”.

Pia alisema watafanya utafiti wa wingi na mtawanyiko wa samaki katika bahari kuu, kutoa leseni 55 kwa meli za uvuvi, kuimarisha taasisi za uvuvi kwa kujenga miundombinu muhimu.

Alisema pia watanunua boti mbili zenye vioo chini ili kuongeza utalii kwenye hifadhi za bahari na maeneo tengefu, kufanya utafiti wa kujua wingi, aina na mtawanyiko wa samaki katika maziwa makuu, Bahari ya Hindi na Bwawa la Nyumba ya Mungu.

Alisema pia watajenga vyumba vitano vya mihadhara na vifaa vya kufundishia katika kampasi tano, ujenzi wa viwanda viwili vya kutengeneza chakula cha samaki na kuchakata mazao ya uvuvi.

Mbali na hotuba ya bajeti, jana wadau mbalimbali wa wizara ya mifugo na uvuvi walionyesha bidhaa zao kwa wabunge na wageni wengine kupitia mabanda maalum yaliyowekwa kwenye viwanja vya Bunge na Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, alitembelea mabanda hayo na kufanya uzinduzi rasmi wa Wiki ya Protini.

Wabunge walianza kuchangia hotuba hiyo jana jioni na kwa mujibu wa ratiba iliyotolewa na Bunge ya shughuli za wiki hii, mjadala huo utaendelea hadi leo ambako Waziri Ulega anatarajiwa kufanya majumuisho baada ya kusikiliza hoja za wabunge watakaochangia.

***SOMA HOTUBA KAMILI UK. 9-16**

## Baadhi waumini waliofungiwa hadi kufa wabainika kuwa walinyongwa

**Na Maulid Mmbaga**

WAZIRI wa Mambo ya Ndani wa Kenya, Kithure Kindiki, amesema uchunguzi wa awali uliofanyika katika miili 110 ya waumini wa Mchungaji Paul Mackenzie umebaini kuwa vifo vya baadhi yao walitokana na kuumizwa na kunyongwa.

Amesema hayo yalibainika baada ya wataalamu wa uchunguzi wa kisayansi kuanzisha upasuaji wa miili iliyopatikana kwenye makaburi yaliyohusishwa na mchungaji huyo anayedaiwa kuwashawishi wafuasi wake kufunga hadi kufa ili wakutane na Mungu.

Waziri huyo alimkariri mtaalamu mkuu wa serikali katika masuala ya upasuaji, Johansen Oduor, kwamba baada ya uchunguzi wa maiti kufanyika, walibaini kuwa wengi wao walikufa kwa ishara za njaa.

“Tuliona ishara za watu ambao hawajala, hakukuwa na chakula tumboni mwao. Pia kiwango cha mafuta mwilini kilikuwa kidogo.

“Kutokana na kile tunachosikia, kulikuwa na dalili kwamba walikufa kwa kufunikwa pua na vinywa vyao, hiyo inaweza kuwa sababu ya kukosa hewa. Hilo lilionekana kwa watoto wawili,” alisema mtaalamu huyo.

Wakati hayo yakiendelea, wachungaji wawili Mackenzie wa Kanisa la Good News International na mwenzake Ezekiel Odero, kiongozi wa Kanisa la New Life Prayer Center, walifikishwa mahakamani kwa madai ya kuhusika na mauaji ya watu wengi katika msitu wa Shakahola, Kaunti ya Kilifi.

Hata hivyo, inaelezwa kuwa kiongozi wa kanisa la New Life Prayer Center, Odero anatuhumiwa kwa mashtaka mbalimbali ikiwamo ya mauaji, utekaji nyara, itikadi kali, uhalifu dhidi ya ubinadamu, ukatili wa watoto, ulaghai na utakatishaji fedha.

Zaidi ya makanisa 4,000 yamesajiliwa nchini Kenya lakini jitihada za kuyaondoa yale yasiyozingatia maadili kupitia udhibiti zimezuiwa kwa madai kwamba ni ukiukwaji wa haki za kikatiba za uhuru wa dini na kuabudu.

**Chanzo: Habari za kimataifa**

# Waziri auawa kwa risasi na mlinzi kisa ujira wake

**KAMPALA,** UGANDA

WAZIRI wa Kazi na Ajira na Uhusiano kazini wa Uganda, Kanali (mstaafu) Charles Engola, ameuawa kwa kupigwa risasi na mlinzi wake, huku baadhi ya mashuhuda wakibainisha kuwa amefanya hivyo kutokana na kucheleweshewa mshahara wake.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Jeshi la Polisi la Uganda, Kanali Engola aliuawa jana asubuhi nyumbani kwake Kyanja, Kampala na mlinzi wake ambaye pia dakika chache baadaye alijiua kwa kujipiga risasi.

Baadhi ya walioshuhudia tukio hilo walisema mlinzi huyo alizunguka katika eneo hilo akifyatua risasi hewani, huku ikibainishwa kuwa baadhi ya watu walijeruhiwa katika tukio hilo.

Naibu Msemaji wa Polisi wa Uganda, Luke Owoyesigire, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo kwa njia ya simu alipozungumza na gazeti la Daily Monitor la nchi hiyo.

"Ndio ukienda Kyanja kuna ufyatuliaji risasi ambao umetokea, mlinzi amemuua mwajiri wake," alisema Owoyesigire.

Spika wa Bunge la Uganda, Anita Among, pia alithibitisha tukio hilo wakati akiendesha kikao cha bunge jana asubuhi.

"Asubuhi hii (jana) nimepokea taarifa za kusikitisha kuwa Mheshimiwa Engola ameuawa kwa kupigwa risasi na mlinzi wake ambaye pia amejiua," alisema Among.

Mmoja wa walioshuhudia tukio, alidai kuwa mlinzi huyo hakuwa amelipwa mshahara wake.

"Mlinzi alisema kuwa hakuwa amelipwa. Alisema ana mke ambaye ni mjamzito na watoto wake hawakuwa wanakwenda shuleni, wakati mwajiri wake alikuwa anakwenda kazini kila siku," alisema mmoja wa mashuhuda hao. **RFI**



Mbunge wa Arumeru Mashariki, Dk. Danielson Pallangyo (kushoto), akimkabidhi cheti Beatrice China Roy katika mahafali ya Chuo cha Ualimu Patandi Arusha mwishoni mwa wiki. Mwalimu huyo analelewa na kujengewa uwezo wa kutimiza ndoto yake na Shirika la Wanawake Katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI) la jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Babu adaiwa kuua wajukuu zake kwa kuwapiga na mchi kichwani

**Na Moses Ng'wat,** SONGWE

JESHI la Polisi mkoani Songwe, linamshikilia Aloyce Nyabwanzo (51), mkazi wa Kijiji cha Kapalala wilayani hapo, kwa tuhuma za kuwaua wajukuu zake wawili kwa kuwapiga kichwani hadi kumwaga ubongo kwa mchi wa kutwangia nafaka.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Songwe, Kamishna Msaidizi (ACP) Theopista Mallya, alisema jana kuwa tukio hilo lilitokea Jumapili iliyopita saa 5:00 usiku. Alisema jeshi hilo linaendelea na uchunguzi ili kujua sababu za mtuhumiwa kutenda tukio hilo.

Alisema mtuhumiwa huyo alitumia mbinu ya kuwavizia wajukuu zake wakati wanatoka chumbani kwao kumfuata bibi yao aliyekuwa sebuleni ndipo akatekeleza mauaji hayo.

"Miili ya watoto hawa imefanyiwa uchunguzi na daktari na kubaini kuwa vifo vyao vimesababishwa na kupasuka kwa mafuvu ya kichwa baada ya kupigwa na kitu kizito hadi ubongo kutoka nje. Hali hiyo imesababisha kuvuja damu nyingi," alisema Kamanda Mallya.

Aliwataja watoto hao waliouawa kuwa ni Jackson Chacha (2) na George Chacha (5) ambao walikuwa wakilelewa nyumbani kwa mtuhumiwa huyo.

Hata hivyo, Kamanda Mallya alisema wakati uchunguzi wa tukio hilo ukiendelea, mtuhumiwa huyo watampeleka hospitalini ili kupimwa afya ya akili.

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

## OMBI LA KUONESHA NIA YA UTOAJI HUDUMA ZA VIFAA VYA OFISINI - KUMBUKUMBU NA. 00000198

Kampuni ya Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) Ltd, ("EACOP LTD") inaalika kampuni zenye uzoefu na weledi wa kutosha kuonesha nia ya kutoa huduma ya vifaa vya ofisini katika Mradi wa EACOP.

Mradi wa EACOP unajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba la kusafirisha Mafutaghafi lililofukiwa chini ya ardhi linalokatisha mipaka ya nchi mbili kwa ajili ya kusafirisha mafuta ghafi katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka rasi ya Chongoleani, katika Mkoa waTanga nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni kilomita 1,443, kati yake kilomita 296 zitakuwa nchini Uganda, na kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI YA MAWANDA YA HUDUMA**

- Mtoa huduma kutoa huduma ya ugavi wa vifaa mbalimbali vya ofisini ikiwemo karatasi, rula, peni, bahasha, vifaa vya kutobolea matundu karatasi pamoja na vifaa vingine vya ofisini vinavyoendana navyo kadri ya mahitaji ya kampuni ya EACOP Ltd.
- Ugavi au utoaji wa vifaa vya ofisini utapaswa kufanyika kwenye ofisi za kampuni ya EACOP Ltd ndani ya siku 3 (Tatu) za kazi tangu kutolewa kwa ombi la Manunuzi.
- Huduma hii itatolewa kwa EACOP Ltd kwa kipindi cha awali cha miaka mitatu.
- Wakati wote mkandarasi atatakiwa kudumisha viwango vya juu zaidi vinavyohitajika katika nyanja zote ikiwa ni pamoja na usafirishaji na ufungashaji mzuri wa vifaa vya ofisini, vifaa vyenye ubora na utoaji wa vifaa vya ofisini ndani ya muda mwafaka.
- Mtoa huduma atawajibika kubadilisha kifaa cha ofisini endapo kitavunjika, hususani kabla na wakati wa kukabidhi vifaa husika.

**VIGEZO MUHIMU:**
**Makampuni au taasisi zinzoonesha nia zinaalikwa kutuma maombi na kuambatanisha nyaraka zifuatazo:**

- Leseni ya biashara.
- Leseni halali, kama ipo, kutoka mamlaka ya ndani ya nchi husika kwa ajili ya utoaji wa huduma husika.
- Uthibitisho wa usajili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na cheti cha mlipa kodi kwa mwaka wa fedha uliopita.
- Waombaji wanasisitizwa sana kuhakikisha kuwa wamejisajili kwenye kazidata ya EWURA (LSSP) ya Watoa Huduma za Ugavi wa Ndani, wakati wa kuwasilisha majibu ya kuonesha nia.
- Kukidhi vigezo na Kanuni za watoa huduma Wazawa za mwaka 2017.
- Uzoefu, utendaji na uwezo wa kutoa huduma zilizoorodheshwa hapo juu katika kiwango kikubwa nchini Tanzania, kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.
- Wasifu wa wafanyakazi muhimu watakaohusika katika mradi ikiwa ni pamoja na vyeti vya lazima vya wahudumu na viwango vya elimu, pamoja na uzoefu na uwezo wa kutoa huduma zinazotakiwa.
- Uwezo wa kifedha wa kutoa huduma zinazohitajika ikiwa ni pamoja na kuwasilisha hesabu za fedha za miaka 3 iliyopita.
- Uthibitisho kutoka kwenye mfumo wa Usimamizi wa QHSE, taasisi na mchakato kulingana na Viwango vya Ndani na vya Ki-Sekta vinavyotumika kwa kazi kama hii.
- Uthibitisho wa kukubaliana na sera za kupiga vita rushwa, ufisadi, na Haki za Binandamu.

Makampuni yenye nia, ambayo yana uwezo na rasilimali za kutosha kutoa huduma zilizotajwa hapo juu yanapaswa kutuma maombi na kuambatanisha nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe ya **procurement.tz@eacop.com** (ukubwa wa barua pepe usizidi **20Mb**) mnamo au kabla ya tarehe **16 Mei 2023** saa **11:00 jioni** kwa saa za Afrika Mashariki (EAT). Kichwa cha Barua pepe kiwe **00000198_ Utoaji wa Huduma wa Vifaa vya Ofisini**.

Maombi yote ya kuonesha nia yawe kati ya kurasa 10 hadi 20.

Maombi yote lazima yawasilishwe kwa lugha ya Kingereza.

**Muhimu:** Kampuni ya EACOP LTD itapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yenye nia kulingana na EOI hii na kufanya tathmini kwa kutumia vigezo vya ndani ili kubaini makampuni yatakayojumuishwa kwenye orodha ya (Makampuni) ya awali yaliyokidhi vigezo. Makampuni yaliyofuzu hatua za awali pekee ndiyo yatakayopewa mwaliko wa zabuni, kwa kutia saini Mkataba wa Kutunza Siri (NDA), kama mwendelezo wa wito wa mchakato wa utoaji wa zabuni. Kampuni ya EACOP LTD inayo haki ya kufanya maamuzi yake ya kuchagua au kukataa kampuni na kubaki na maamuzi yake pasipo kutoa sababu kwa kampuni husika.

RIPOTI YA UCHUNGUZI

# Madhara reli hifadhini yaipa funzo serikali

## •Treni mbugani sasa kupita juu, mahandaki

**Na Mwandishi Wetu**

"USILETE mnyama, mmea au kitu chochote katika hifadhi". Hii ni moja ya Kanuni 15 za Kusimamia Usalama wa Mbuga ya Saadani inayopatikana katika halmashauri nne; Bagamoyo na Chalinze za Mkoa wa Pwani, Pangani na Handeni za Mkoa wa Tanga.

Ni Hifadhi ya Taifa ya 13 kuanzishwa nchini miongoni mwa 22 zinazosimamiwa na Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA). Ina ukubwa wa kilomita za mraba 1,100.

Kanuni zake za usalama zinapiga marufuku kelele; kulima hifadhini; kuchuma maua au kukata mimea; kuwasha moto; kuwinda wanyamapori na hata kusikiliza muziki kwa njia ya redio au simu.

Hifadhi ya Taifa Saadani (SANAPA) ni mbuga yenye sifa ya kuwa na aina zaidi ya 60 za wanyamapori, aina zaidi ya 270 za ndege na wingi wa mamba na viboko.

Hata hivyo, tayari imeelezwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Charles Kichere, kupitia ripoti yake ya mwaka 2020/21, kwamba uendelevu wake uko shakani kutokana na kuingiliwa na shughuli za kibinadamu zinazojumuisha uchimbaji madini na kilimo cha miwa.

Kukiwa na hoja hiyo ya CAG, Nipashe inaona kikwazo kingine - reli ya Shirika la Reli Tanzania (TRC) imepita katikati ya hifadhi, ikiigawa mbuga hiyo vipande viwili.

Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi wa SANAPA, Ephraim Mwangomo, anabainisha kuwa urefu wa kipande cha reli kilichomo ndani ya hifadhi, kwa reli inayotoka Dar es Salaam kwenda Arusha, ni kilometa 54. Hii ni kuanzia Mto Wami wilayani Bagamoyo katika Mkoa wa Pwani hadi Kijiji cha Mkalamo, Wilaya ya Pangani mkoani Tanga.

Kwa utafiti wa Nipashe, hakuna rekodi zozote nchini juu ya utafiti rasmi uliokwishafanywa kubaini athari za kujengwa kwa reli na kupita kwa treni katika Hifadhi ya Saadani na kuja na mapendekezo ya kubadili mfumo wa sasa.

"Kule Hifadhi ya Taifa Mikumi (MINAPA) tayari kuna utafiti umefanyika wa kubaini madhara ya barabara ya lami kupita hifadhini. Hapa kwetu (SANAPA) bado hakuna utafiti wa aina hiyo," Kamishna Mwangomo anaeleza.

"Lakini ufuatiliaji wetu umebaini wanyamapori wamezoea kuona treni inapita hifadhini. Awali waliposikia honi ya treni, walitimua mbio. Sasa hawaiogopi tena, wanasogea karibu na reli lakini hawaendi pale katikati, wanajua kuna 'jitu' kubwa linapita hapa. Wanyamapori ni wepesi sana kubadilika," anafafanua.

Kamishna Mwangomo pia anabainisha kuwa treni inapokuwa hifadhini, "haigongwi bali inagonga. Ikitokea ajali ya mnyama kugongwa au treni kupata ajali hifadhini, basi dereva wake (kandawala) anatozwa faini kulingana na thamani ya mnyama aliyemgonga na faini kwa kusababisha ajali hifadhini."

Ili kuzuia ajali za treni kugonga wanyamapori, Kamishna Mwangomo anasema wanashirikiana na TRC kudhibiti tabia hatarishi za kandawala na abiria wake hifadhini; akiutaja mwendo elekezi wa treni hifadhini ni kilometa 50 kwa saa.

Anasema huo ni mwendo unaowezesha abiria kuona wanyamapori mbugani nyakati za mchana; tena bila kulipa chochote kwa SANAPA.




Wataalamu wanasema treni kupita hifadhini kuna madhara kiikolojia.

"Kabla ya kuingia hifadhini, dereva wa treni (kandawala) anatia saini kibali maalum cha kupita hifadhini na kuahidi kwamba atazingatia taratibu na kanuni za usalama hifadhini. Akitoka hifadhini, anatia saini tena, katika stesheni inayofuata, kwamba 'nimepita hifadhini kwa kuzingatia taratibu zilizowekwa'.

"Pia kunatolewa matangazo kwa abiria kwamba 'sasa tunaingia hifadhini, huruhusiwi kutupa chochote, hata kuwapa chakula wanyamapori'," anaeleza.

Ni masharti ambayo Kamishna Mwangomo anayataja yamesaidia kuepuka ajali za wanyamapori kugongwa na treni. Anasema tukio la ajali mwisho hifadhini likihusisha mnyama mkubwa ni la mwaka 2001, nyati alipogongwa na treni.

Hata hivyo, Profesa wa Mifumo ya Ikolojia, Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA) Idara ya Mifumo Ikolojia na Uhifadhi, Pantaleo Munishi, amemwambia mwandishi kuwa madhara ya kupitisha reli hifadhini hayakomei kwenye kujeruhi au kuua wanyamapori, bali kuigawa pia hifadhi vipande viwili na kuharibu mfumo wa ikolojia.

Prof. Munishi anasema reli hiyo inakuwa kizuizi kwa viumbe hai kujongea kutoka eneo moja hadi lingine. Inatenga mikusanyiko ya wanyamapori na ndege wasio na uwezo mkubwa wa kuruka.



Mwaka 2001, nyati aligongwa na treni hifadhini Saadani.

"Kuzaliana kwao kunakuwa kwa shida. Kuna wanyama ambao wanahitaji eneo kubwa, ukishapitisha reli na kuigawa hifadhi vipande, unavuruga kuzaliana kwao.

"Pili, kuna madhara ya moja kwa moja treni inapogonga na kuua wanyama. Kama aliyegongwa yuko kwenye kundi la viumbe adimu, maana yake aina hiyo ya mnyama inatoweka. "Tatu, kuna hatari reli ikajengwa eneo ambalo ni mahususi kwa ustawi wa aina adimu za wanyamapori. Hali hiyo ikishatokea, mnyama huyo hawezi kuishi tena," Prof. Munishi anafafanua.

Mtaalamu huyo pia anasema treni inasababisha kelele hifadhini, akifafanua kuna wanyama hawapendi kelele, hivyo watahama.

"Kule inakopita reli, kuna mimea imeondolewa. Treni inapopita hifadhini, abiria wake wanatupa taka. Ushauri wangu: maeneo ambayo ni tengefu yaachwe, yabaki kama yalivyo, yalindwe na yatunzwe.

"Kama kuna eneo la hifadhi liliingiliwa na shughuli za kibindamu, ziondolewe. Sheria zipo, tuzitii. Tuna Sheria ya Misitu; Sheria ya Wanyamapori ipo; Sheria ya Hifadhi za Taifa ipo. Zote zinakataza shughuli za kibinadamu hifadhini. Tuzitii," anashauri.

Ofisa Miradi wa Timu ya Wanasheria Watetezi wa Mazingira kwa Vitendo (LEAT), Clay Mwaifwani, anaungana na Prof. Munishi kwamba, ujenzi wa reli na uendeshaji wa huduma za usafirishaji ndani ya hifadhi unaweza kusababisha kugawanyika kwa makazi ya wanyamapori.

Anabainisha ni hatari inayowaathiri zaidi wanyamapori wadogo ambao hushindwa kujongea kutoka sehemu moja kwenda nyingine.

"Kwa maneno mengine ni kuwa, reli na usafirishaji unaigawa hifadhi kwa kutengeneza hifadhi ndani ya hifadhi.

"Baadhi ya maeneo ndani ya hifadhi huwa na umuhimu wa kipekee kiikolojia. Wanyama hupendelea maeneo hayo kwa sababu huwa na mazingira wezeshi kwao kuzaliana au kulea watoto wao mpaka watakapoweza kuyamudu mazingira mengine," anaeleza.

Mwaifwani anaitaja hoja nyingine anayosisitiza inapaswa kuzingatiwa, ni utafiti wa ulinzi wa mazingira kabla ya kutekeleza mradi wa ujenzi wa reli na usafirishaji ndani ya eneo hilo ambalo awali lilikuwa pori la akiba na baadaye mwaka 2005 likatangazwa kuwa hifadhi ya taifa.

Anasema utafiti wa kimazingira ufanyike ili kujua athari kwa ikolojia ya hifadhi zinazoweza kusababishwa na mradi wa reli na namna ya kuziepuka au kuzidhibiti.

"Kwa mfano, ujenzi wa reli unaweza kuhusisha ujenzi wa mahandaki ama madaraja ya juu ili kuepuka na kudhibiti athari kwa mazingira na ikolojia ya hifadhi.

"Je, kwa wakati uliopo, TRC wanafanya ukaguzi wa mazingira kila mwaka kujua athari za usafirishaji ndani ya eneo la hifadhi? Taasisi nyingine kama NEMC (Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira) na TANAPA wanalindaje ikolojia ya hifadhi? Majibu ya ukaguzi wa mazingira yanatuonesha nini? Hifadhi iko salama kiasi gani?" Mwaifwani anahoji.

Mkurugenzi Mkuu wa TRC, Masanja Kadogosa, anakiri treni kupita hifadhini ni hatari kwa ustawi wa wanyamapori na uendelevu wa ikolojia ya hifadhi.

Hata hivyo, anabainisha hawana mkakati wa kuiondoa reli katika Mbuga ya Saadani, lakini sasa wanauzingatia ustawi wa hifadhi wanapotekeleza miradi mipya ya reli inayoendelea nchini.

"Reli inayopita Saadani ni ya kizamani. Inahitaji bajeti kubwa kuibadilisha kwa maana ya kuipitisha chini kwenye mahandaki au juu ili kutoleta usumbufu kwa viumbe hifadhini. Reli ya kisasa inakuwa na uzio.

"Lakini hili limetupa somo. Miradi yote ya reli inayoendelea sasa tunazingatia sana suala hili. Mfano, reli kutoka Arusha kwenda Musoma itakapofika eneo la Hifadhi ya Taifa Serengeti, itapita juu kabisa, yaani wanyama hawatosumbuliwa kabisa," anafafanua.

Kukabiliana na madhara ya miundombinu ya reli na kupita kwa treni hifadhini Saadani, Kadogosa anasema wanayo mikakati mbalimbali inayojumuisha kupiga honi pale treni inapokuwa hifadhini, wana alama za tahadhari kwa uvukaji wa wanyamapori, watu na magari - maarufu 'W' na mwendo elekezi wa usiozidi kilometa 50 kwa saa.

**USULI**

Inaporejewa historia ya reli nchini, chini ya utawala wa Uingereza, Reli ya Usambara iliunganishwa na reli ya Kenya-Uganda maeneo ya Voi na Moshi kisha kuunganishwa na Arusha mwaka 1929, yaani miaka 94 iliyopita.

Baada ya Uhuru wa Tanganyika, Reli ya Usambara iliunganishwa na Reli ya Kati maeneo ya Ruvu mkoani Pwani na Mruazi wilayani Korogwe mkoani Tanga.

Reli ya Usambara ilikuwa sehemu ya Reli ya Afrika Mashariki (EAR) chini ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, iliyoundwa na nchi za Kenya, Tanzania na Uganda.

Mnamo mwaka 1977, jumuiya hiyo ilivunjika na Reli ya Usambara ikawa sehemu ya mgawo ilioupata Tanzania kutoka mali za jumuiya.

SANAPA ilianzishwa miaka 18 iliyopita kwa Tangazo la Serikali Na. 281 la Septemba 16, 2005 baada ya kupandishwa hadhi kwa Pori la Akiba Saadani lililoanzishwa kisheria mwaka 1968.

Hii ina maana kwamba, wakati reli inajengwa kutoka Ruvu kwenda mikoa ya kaskazini mwa nchi, baada ya Uhuru wa Tanganyika, tayari eneo la Saadani inamopita reli hiyo, lilikuwa hifadhi yenye wanyamapori, hivyo mradi wa reli ulipaswa kuzingatia maslahi ya uhifadhi wa wany-

# Saratani sasa tishio watoto, vijana

**Na Christina Mwakangale**

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili (MNH) imesema kwa mwaka imekuwa ikipokea wagonjwa wapya wa saratani takribani 500 ambao ni watoto walio na umri wa balehe wa miaka 14 na 15.

Mkurugenzi Mtendaji wa MNH, Prof. Mohamed Janabi, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, kwenye mafunzo yaliyolenga kuwaongezea ujuzi wauguzi hasa wanaotoa huduma kwa watoto wanaougua ugonjwa huo.

Prof. Janabi alitaja baadhi ya sababu zinazochangia watoto hao kuugua saratani kuwa ni pamoja lishe duni inayoegemea zaidi mlo wa sukari na wanga na unene kupindukia. Akisema changamoto kwa ugonjwa huo ni namna ya kuugundua mapema.

"Watoto wanaougua ugonjwa huu ni vijana wanaokua, walioko kwenye umri wa miaka 14 na 15 kushuka chini ambao matibabu yao yanahitaji uangalizi na namna ya kutumia dawa. Duniani kwa ujumla tuna kesi mpya 800,000 kila mwaka. Nizungumzie kwetu (MNH) tuna kesi mpya kabisa 500 za saratani kwa watoto kila mwaka.

"Mafunzo kama haya ni muhimu kwa sababu mtoto mwenye saratani huduma zao ziko tofauti, mafundisho haya ni ya namna wauguzi wanaweza kuhudumia, tunashukuru kwa mafunzo haya ambayo wanufaika watakwenda kufundisha wenzao,"alisema Prof. Janabi.

Pia alisema kuna dhana iliyojengeka kwamba wanaougua ugonjwa huo ni watu wazima na si watoto huku akisema nao huugua ikiwamo saratani ya damu, mifupa na ini.

Alisema hospitali hiyo ina wodi maalumu kwa ajili ya matibabu hayo, kuna vitanda 30 kwa ajili ya wanaolazwa.

"Wengi wa wagonjwa hawa wanatoka katika familia za chini. Hata familia zenye uwezo wa kati bado dawa bei zake ni kubwa, vipimo ni ghali, hivyo serikali inachangia sehemu kubwa katika matibabu haya. Lakini elimu katika matibabu haya ni silaha kubwa na MNH tuko tayari kuhudumia," alisema Prof. Janabi.

Kuhusu mbinu za kujikinga, Prof. Janabi alisema baadhi ya saratani zinazogundulika kwa watoto, zinaweza kuzuilika na kwamba, tatizo kubwa ni elimu duni miongoni mwa jamii, hususani suala la mlo wa kila siku.

Mkurugenzi Msaidizi wa Huduma za Kitabibu za Uuguzi na Ukunga kutoka Wizara ya Afya, Paul Magesa, alisema kutokana na tatizo kuwa bado ni kubwa, wizara imeelekeza nguvu katika kuzuia kwa kutoa elimu.

"Huduma ya saratani kwa ujumla wake sasa inatolewa ORCI (Taasisi ya Saratani Ocean Road), MNH na Hospitali za Benjamin Mkapa na Bugando, lengo ni ili huduma ziwafikie wagonjwa pale walipo," alisema.


## SHIRIKA LA UMEME TANZANIA

TANESCO

# TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Wananchi wote mnatangaziwa kwamba, SHIRIKA LA UMEME TANZANIA (TANESCO) litaondosha kwa njia ya mnada wa hadhara Magari, Pikipiki za matairi mawili, Vyuma Chakavu, Vifaa vya Umeme/scraps na vifaa mchanganyiko mbalimbali katika Mikoa ya Tanzania bara kama inavyoonekana hapa chini:

**MKOA WA DAR ES SALAAM**

| S/NO | TAREHE | IDADI YA SIKU | KITUO | AINA YA MALI |
|---|---|---|---|---|
| 1 | 16/05/2023 | 1 | A. BAHARI BEACH | NYAYA ZA UMEME CHAKAVU |
| | | | B. KURASINI CENTRAL STORE | VIFAA CHAKAVU MCHANGANYIKO |
| 2 | 17/05/2023 | 1 | TEMEKE | VIFAA CHAKAVU MCHANGANYIKO |
| 3 | 18/05/2023 | 1 | ILALA | VIFAA CHAKAVU MCHANGANYIKO |
| 4 | 19/05/2023 | 1 | KINONDONI KUSINI | VIFAA CHAKAVU MCHANGANYIKO |
| 5 | 20/05/2023 | 1 | KINONDONI KASKAZINI | VIFAA CHAKAVU MCHANGANYIKO |

| S/NO | MKOA | TAREHE | KITUO | AINA YA MALI |
|---|---|---|---|---|
| 1 | PWANI | 22/05/2023 | CHALINZE | VIFAA CHAKAVU MCHANGANYIKO |
| 2 | LINDI | 25/05/2023 | LINDI | VIFAA CHAKAVU MCHANGANYIKO |
| 3 | MTWARA | 27/05/2023 | MTWARA | VIFAA CHAKAVU MCHANGANYIKO |
| 4 | SONGEA | 30/05/2023 | SONGEA | VIFAA CHAKAVU MCHANGANYIKO |
| 5 | NJOMBE | 01/06/2023 | NJOMBE | VIFAA CHAKAVU MCHANGANYIKO |
| 6 | IRINGA | 03/06/2023 | IRINGA | VIFAA CHAKAVU MCHANGANYIKO |
| 7 | MBEYA | 05/06/2023 | MBEYA | VIFAA CHAKAVU MCHANGANYIKO |
| 8 | SUMBAWANGA | 07/06/2023 | SUMBAWANGA | VIFAA CHAKAVU MCHANGANYIKO |
| 9 | KATAVI | 09/06/2023 | KATAVI | VIFAA CHAKAVU MCHANGANYIKO |
| 10 | KIGOMA | 12/06/2023 | KIGOMA | MAGARI NA VIFAA CHAKAVU MCHANGANYIKO |
| 11 | KAGERA | 15/06/2023 | KAGERA | MAGARI NA VIFAA CHAKAVU MCHANGANYIKO |
| 12 | GEITA | 17/06/2023 | GEITA | VIFAA CHAKAVU MCHANGANYIKO |
| 13 | MWANZA | 19/06/2023 | MWANZA | VIFAA CHAKAVU MCHANGANYIKO |
| 14 | MUSOMA | 21/06/2023 | MUSOMA | MAGARI NA VIFAA CHAKAVU MCHANGANYIKO |
| 15 | SIMIYU | 23/06/2023 | SIMIYU | VIFAA CHAKAVU MCHANGANYIKO |
| 16 | SHINYANGA | 26/06/2023 | SHINYANGA | VIFAA CHAKAVU MCHANGANYIKO |
| 17 | TABORA | 28/06/2023 | TABORA | VIFAA CHAKAVU MCHANGANYIKO |
| 18 | SINGIDA | 17/07/2023 | SINGIDA | MAGARI, PIKIPIKI NA VIFAA CHAKAVU MCHANGANYIKO |
| 19 | DODOMA | 19/07/2023 | DODOMA | MAGARI, PIKIPIKI NA VIFAA CHAKAVU MCHANGANYIKO |
| 20 | MOROGORO | 21/07/2023 | MOROGORO | MAGARI, PIKIPIKI NA VIFAA CHAKAVU MCHANGANYIKO |
| 21 | TANGA | 24/07/2023 | TANGA | MAGARI NA VIFAA CHAKAVU MCHANGANYIKO |
| 22 | MOSHI | 26/07/2023 | MOSHI | VIFAA CHAKAVU MCHANGANYIKO |
| 23 | ARUSHA | 28/07/2023 | ARUSHA | MAGARI NA VIFAA CHAKAVU MCHANGANYIKO |
| 24 | MANYARA | 31/07/2023 | MANYARA | VIFAA CHAKAVU MCHANGANYIKO |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Chombo/Kifaa kitauzwa kama kilivyo na mahali kilipo;
2. Mnunuzi atalazimika kulipa papohapo amana (deposit) isiyopungua asilimia ishirini na tano (25%) ya thamani ya Chombo/Kifaa alichonunua, na kukamilisha malipo yote katika muda wa siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya mnada. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti hili atakosa haki zote za ununuzi wa Chombo/kifaa husika na amana iliyolipwa haitarudishwa;
3. Mtu yeyote atae tamka bei ya juu kisha akashindwa kulipa asilimia ishirini na tano (25%) ya bei aliyotamka, atachukuliwa kuwa ni mwenye kutaka kuvuruga mnada na hivyo hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake kwa mujibu wa sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
4. Mnunuzi atatakiwa kuondoa/kuchukua chombo alichonunua katika muda wa siku saba (7) kuanzia siku ya kukamilisha malipo; Mnunuzi atakayechelewa kuondoa/kuchukua chombo/kifaa chake atatakiwa kulipia gharama za uhifadhi wa chombo/kifaa hicho ambayo ni asilimia 0.5 (0.5%) ya gharama ya chombo/kifaa kwa siku.
5. Vyuma Chakavu vitauzwa kwa Wanunuzi wenye viwanda vya kuchakata chuma tu. Wanunuzi wa vyuma chakavu watatakiwa kuleta leseni za kuchakata chuma na leseni hizo zitakaguliwa kabla ya zoezi la mnada kuanza. Vile vile nakala ya leseni hiyo itabaki kwa Muuzaji kwa ajili ya kumbukumbu;
6. Gharama za kubadilisha umiliki ni jukumu la mnunuzi na atatakiwa kukamilisha taratibu za kumilikishwa chombo/kifaa/chuma chakavu alichonunua kwa mujibu wa Sheria ndani ya siku ishirini na moja (21);
7. Ruhusa ya kuangalia vyombo itatolewa siku (5) kabla ya tarehe ya mnada husika;
8. Mnada utaanza saa nne (04:00) kamili asubuhi katika kila kituo kwa mtiririko ulionyeshwa. Kwa vituo vyenye vituo vidogo yani A and B; mnada utaanza kituo A kufuatia kituo B.
9. Wananchi wote mnakaribishwa kushiriki katika mnada huu wa hadhara.

**IMETOLEWA NA**
**MKURUGENZI MTENDAJI**
**SHIRIKA LA UMEME TANZANIA (TANESCO)**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kila mdau atimize wajibu kuhimiza uhuru wa habari

**LEO** ni Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari ambayo inakwenda sambamba na maadhimisho ya miaka 30 tangu ilipotangazwa rasmi na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa (UNGA) kuwa siku rasmi ya Uhuru wa Vyombo vya Habari Duniani (WPFD). Lengo la kuwapo kwa maadhimisho hayo ni kuhakikisha uhuru huo unapewa kipaumbele huku waandishi na wanahabari wakithaminiwa na kutambuliwa.

Ni dhahiri kwamba Umoja wa Mataifa ulipitisha siku hii kutokana na nafasi ya vyombo vya habari katika jamii na kwenye nyanja zote za kimaisha, yaani kisiasa, kiuchumi na kijamii. Kutokana na umuhimu huo, vyombo vya habari vina nafasi kubwa kwa sababu ya wajibu wake katika kuhabarisha, kuelimisha na kuburudisha.

Kwa sababu ya dhima hiyo na nafasi yake, vyombo vya habari katika mataifa mbalimbali duniani vimepewa hadhi ya kuwa mhimili wa nne (usio rasmi) nje ya ile inayojulikana ambayo ni Bunge, Utawala na Mahakama.

Hii inajidhihirisha wazi kutokana na ukweli kwamba taasisi mbalimbali za kisekta, wakiwamo wanasiasa na watu binafsi, wamekuwa wakitumia vyombo vya habari kwa ajili ya kuupasha umma kuhusu kinachoendelea ndani ya asasi hizo. Hiyo ni kutokana na si kuthamini tu vyombo vya habari bali wanaamini kwamba vimebeba dhima kubwa ya kufikisha ujumbe kwa jamii na kwa haraka.

Ili kuhakikisha vinafanya kazi ipasavyo na kwa kufuata sheria, miongozo na taratibu zinazoongoza nchi, vyombo vya habari vimetungiwa sheria na kanuni kulingana na matakwa ya kinchi. Tanzania ni mfano wa kuwepo kwa sheria hiyo baada ya vyombo vya habari kutungiwa Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari ya mwaka 2016 licha ya kwamba inalalamikiwa kuwa ni kandamizi na wadau kutaka ifanyiwe marekebisho.

Pamoja na kuwapo kwa sheria hizo katika nchi mbalimbali, kwa kiasi kikubwa imekuwa ikidaiwa kuwa uhuru wa vyombo vya habari unaminywa na watawala hivyo kuwafanya wanahabari kushindwa kufanya kazi zao kwa ufanisi na mazingira rafiki. Pia ni ukweli usiopingika kwamba baadhi ya taasisi zimeviteka vyombo vya habari hivyo kushindwa kuripoti madudu yanayotokea katika taasisi husika.

Kutokana na kuwapo kwa mazingira hayo, ni vyema wanahabari wakiwamo wahariri wa vyombo vya habari, vyama vya kitaaluma na wadau wanaokutana Zanzibar kwenye maadhimisho ya mwaka huu, wakatumia fursa hiyo kujadili changamoto hizo na kuzitafutia ufumbuzi.


Yako mambo mengi ambayo yamekuwa kikwazo kwa uhuru wa vyombo vya habari yakiwamo unyanyaswaji, kupigwa, kunyang'anywa vifaa na kutishiwa kama 'ajali kazini'. Madhara mengine makubwa zaidi ambayo yamewakuta wanahabari ni pamoja na kujeruhiwa, kutekwa au kupoteza maisha.

Nchini Tanzania, kwa mfano, takribani miaka saba iliyopita baada ya kuwapo kwa Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari ya Mwaka 2016 baadhi ya vyombo vya habari vimekumbwa na madhila mbalimbali kama vile kutishiwa, kukamatwa, kufungiwa, kutekwa, kuingiliwa kwa uhuru wa uhariri, kupigwa faini kwa chombo cha habari, vifo, kuharibiwa vifaa vya kazi, kuondolewa katika eneo la tukio kinyume cha sheria na kujidhibiti (self-censorship).

Pamoja na hayo, nchini Tanzania kuna nuru na mwanga kwa kuwapo kwa uhuru wa vyombo vya habari kama ambavyo serikali imekuwa ikihimiza na wanahabari kuhakikishiwa kutokuwapo kwa vitisho wala unyanyasaji. Pia serikali imetoa ahadi kwamba kutafanyika marekebisho ya sheria ya sasa inayolalamikiwa kuwa ni kandamizi.

Kwa mantiki hiyo, wadau waliokusanyika Zanzibar kwa ajili ya maadhimisho ya Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari wakajadili kwa kina nini kinachotakiwa kufanyika ili uhuru unaodaiwa upatikane. Hata hivyo hakuna uhuru usio na mipaka, hivyo wadau hao wahimize pia waandishi wa habari kufanya kazi kwa weledi na kufuata maadili.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Walioko ndani na nje ya taaluma habari, wote waepuke hali ya kuvitumia vibaya

Na Halfani Chusi

**MAADHIMISHO** ya Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari, hufanyika kila ifikapo Mei 3 ya mwaka, ambao wanataaluma na wadau hupata nafasi ya kujadili mambo kadhaa, ikiwamo changamoto zinazovikabili vyombo hivyo au wanahabari wenyewe.

Tunapoadhimisha siku hii, muhimu ni kwamba kuna mambo kadhaa ya kuyaangazia ambayo miongoni mwao yanaweza kuwa tishio kwa vizazi, pia yapo mengine yanatumika kurudisha nyuma taaluma ya habari hapa nchini.

Taaluma ya habari ni miongoni mwa fani ambazo zina umuhimu wake mkubwa kwa jamii, kwa kuwa pamoja ndiyo inayochochea maendeleo ya nchi kwenye sekta mbalimbali.

Kaulimbiu ya mwaka huu ni kwamba 'kuunda mustakabali wa uhuru wa kujieleza kama kichocheo cha haki za binadamu." Hii inaonyesha kuna vizuizi vimewekwa kwenye taaluma hii, ikilenga kuminya kuzungumzia baadhi ya mambo ambayo mengine ni wazi yanakwamisha hatua za maendeleo.

Hivyo, inatoa nafasi ya kutafakari suluhisho la kuondoa vikwazo vilivyopo, kwa kuwa upashanaji habari, ni miongoni mwa haki mojawapo ambayo pia ipo kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano.

Kaulimbiu hiyo ni nzuri, lakini vyombo vya habari vinapaswa pia kuwa makini, visitumike vibaya na kusababisha migogoro ya mmomonyoko wa maadili. Wanahabari wamefunzwa namna nzuri ya kuwasilisha hoja mbalimbali, kwa niaba ya jamii (voice of voiceless), pia kuelimisha, kuburudisha na kukosoa pale panapoonekana kuwa na makosa.

Suala la kuandika habari ambazo zinaepusha uvunjifu wa amani, pamoja na kutambua uwepo wa mila na tamaduni na sheria mbalimbali pamoja na katiba lina umuhimu wake.

Hivi karibuni, kumeibuka kampeni isiyo rasmi ya kuhamasisha uhusiano wa jinsia moja yaani ushoga na usagaji, ambao ni kinyume na maadili ya Kitanzania, pia kuna sheria ambazo zinakataza uhusiano wa namna hiyo.

Vyombo vya habari, hapo vina nafasi kubwa katika kuisaidia jamii kutambua madhara ya uwepo wa uhusiano wa jinsi moja, ikiwamo kuathirika kimwili na kisaikolojia, pia kutokuwa na nafasi ya moja kwa moja ya kuzalisha nguvu kazi (kuzaa watoto).

Mbaya zaidi ni kwamba, baadhi ya nchi zenye nguvu ya kiuchumi ndiyo zinahusika katika kufanya kampeni ya jambo hili, huku wakitumia kivuli cha haki za binadamu, hivyo kutishia nchi maskini kuzinyima misaada iwapo hawataridhia jambo hilo.

Ni jambo la kushangaza kwa kuwa wanafumbia macho pia kuvunjwa kwa haki za malezi ya watoto kutokana na uhusiano huu wa jinsia moja ambao wamekuwa wakitumia fedha zao kuasili watoto jambo ambalo linasababisha mkanganyiko wa nafasi ya mzazi ama mlezi.

Japo pia kuna baadhi wanandoa wa jinsia tofauti wapo ambao kutokana na matatizo yaliyo nje ya uwezo wao, wameshindwa kupata hivyo uasili watoto, lakini hawa ni wazi wanakuwa kwenye maadili mtoto anamwita mama mwenye jinsi ya 'Ke' na baba mwenye jinsia ya 'Me'.

Watu waliojiingiza kwenye uhusiano ule mbaya, wakipaswa kusaidia kupewa elimu, pamoja na kufanyiwa maombi au dua, hata kutibiwa kama inabidi, waweze kuachana na tabia hizo.

Jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia, ni kwa wamiliki na viongozi wenye maamuzi kwenye baadhi ya vyombo vya habari wanatumika kuminya nafasi nzuri ya wanataaluma kuitumikia vyema jamii kupitia elimu waliyonayo kwa kuamua kuajiri watu wasio wanataaluma.

Ni vema wamiliki na viongozi wa vyombo vya habari, wakatambua umuhimu wa kuwaajiri au kuwatumia wanataaluma husika kwenye eneo husika, ili kulinda heshima ya fani hii na kutambua tofauti iliyopo kati ya mwanataaluma na mtu tu ambaye ana uwezo wa kuandika ama kuzungumza vizuri.

Taaluma ya habari machoni pa baadhi ya watu, wanaweza kuitazama kama ni kazi rahisi, kwa kuwa inahusisha kuandika ama kuzungumza jambo ambalo kila mtu aliyepata nafasi ya kwenda shule ama ana uwezo wa kuzungumza ama kutumia lugha ya alama.

Ukweli ni kwamba taaluma ya habari ni nyeti inaweza kusababisha maendeleo lakini pia kuleta majanga ikiwamo ya vita, au mmomonyoko wa maadili kwenye jamii, hivyo umakini unahitajika ili kuzuia mabaya kujitokeza.

# Wabunifu 700 nchini waomba mtaji CRDB

**Na Mwandishi Wetu**

UKIWA umepita mwezi mmoja wa kuwatambua wabunifu wanaotaka kuendeleza miradi yao, Benki ya CRDB imepokea zaidi ya maombi 700 ya wajasiriamali wanaotaka mitaji.

Taarifa hiyo ilitolewa jana jijini Dar es Salaam na Kaimu Mkurugenzi wa Mawasiliano wa Benki hiyo, Emmanuel Kiondo alipozungumza na waandishi wa habari.

"Ninapenda kuwajulisha kuwa hadi Aprili 12 dirisha la maombi lilipofungwa, jumla ya maombi 709 yalipokewa yakiwamo 369 yaliyopitia COSTECH na 340 kupitia ICTC. Kipekee kabisa nimshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa kwa kutupa heshima ya kutuzindulia na kutufungulia dirisha la maombi kwa vijana na wanawake alioufanya Machi 12, mwaka huu," alisema Kiondo.

Tangu kuzinduliwa kwa Programu ya Imbeju yenye kaulimbiu ya "Mtaji Wezeshi kwa Vijana na Wanawake" inayotekelezwa kupitia Taasisi ya CRDB Bank Foundation, dirisha la kupokea maombi ya wabunifu wanaomiliki biashara changa lilifunguliwa ili kuwawezesha kwa mtaji, ujuzi wa kitaaluma na masoko vijana na wanawake wanaozimiliki.

Kupokea maombi, Kiondo alisema ilikuwa ni hatua ya kwanza inayohusisha kutoa mafunzo, ushauri na mitaji wezeshi kwa kushirikiana na Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) na Tume ya TEHAMA (ICTC). "Katika kipindi cha mwezi huo mmoja, vijana walipewa fursa ya kuwasilisha maombi ya ushiriki. Maombi yalipokewa kutoka mikoa yote. Asilimia 70.6 ya maombi yaliyopokewa yalitoka kwa vijana wanaume na asilimia 29 yalikuwa ya wanawake. COSTECH imeyapitisha maombi 116 na ICTC 80," alisema Kiondo.

Kaimu mkurugenzi huyo alifafanua kuwa sekta ya kilimo ambayo ni uti wa mgongo wa taifa, imeongoza kwa kuwa na asilimia 31 ya maombi yote ikifuatiwa na sekta ya uzalishaji yenye asilimia 14 huku biashara ya mtandaoni ikichukua asilimia 18 ya maombi yakifuatiwa kwa karibu na sekta ya teknolojia ya masuala ya fedha (asilimia 13).

Mkurugenzi wa Ubunifu na Teknolojia kutoka COSTECH, Dk. Gerald Kafuku alisema ukosefu wa mtaji ndicho kikwazo cha wabunifu wengi kuingiza bidhaa zao sokoni, hivyo aliishukuru Benki ya CRDB kwa kufungua milango ili kuwawezesha.

"Kwa kawaida, COSTECH huwa inatoa ruzuku ya kuendeleza mawazo ya wabunifu. Kwa hatua hii inayotekelezwa na Imbeju, ni kwamba wabunifu wapo tayari kuingia sokoni na wanachokihitaji ni mtaji wa uzalishaji. Kwa muda mrefu, wabunifu hawa walikuwa hawakopesheki kutokana na kutokuwa na dhamana, Ninaishukuru Benki ya CRDB kwa kuwaondolea kikwazo hicho," alisema Dk. Kafuku.

Jason Ndaguzi, Kaimu Mkurugenzi wa Utafiti na Maendeleo ya TEHAMA wa Tume ya TEHAMA, alisema wamepata uzoefu mkubwa na wa aina yake wakati wa kuyachakata maombi ya wabunifu walioujitokeza, hivyo wataboresha mikakati yao ili kukuza zaidi ubunifu nchini.

# Waziri aipongeza GGML kutoa ajira na zabuni kwa Watanzania

**Na Mwandishi Wetu,**
MOROGORO

NAIBU Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu, Patrobas Katambi, ameipongeza Kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML) kwa kutoa fursa za ajira kwa Watanzania ndani ya mgodi huo na kuwapatia wazawa fursa za kutoa huduma za kuuza bidhaa za ndani kwa mgodi.

Pia ameipongeza kampuni hiyo kwa kuibuka Mshindi wa Ubunifu na Banda Bora kwenye maonyesho ya afya na usalama mahali pa kazi yaliyofanyika katika viwanja vya Tumbaku mkoani Morogoro kuanzia tarehe 26 hadi 30 Aprili mwaka huu.

Katambi alitoa pongezi hizo alipotembelea banda la kampuni hiyo katika maonyesho hayo yaliyoratibiwa na Wakala wa Afya na Usalama Mahali pa Kazi (OSHA).

"Niwapongeze hasa kwa kupunguza ulemavu kazini, magonjwa yanayotokana na kazi lakini kuhakikisha kwamba mazingira yote ya kufanyia kazi yanakuwa salama.

"Ninafurahi kuona kwamba banda zima na hata ndani ya kampuni asilimia kubwa ya wafanyakazi ni Watanzania wenzetu. Kwa maana hiyo tunazidi kusisitiza kwamba kwenye maeneo yote ya kazi Watanzania ni kipaumbele," alisema.

Naibu Waziri huyo alisema mgeni anaposhika nafasi ya ajira ina maana kwamba ujuzi huo ni adimu, Mtanzania hana sifa wala vigezo lakini pamoja na hilo, Rais Samia Suluhu Hassan ameelekeza Watanzania wajengewe uwezo kushika nafasi hizo.

"Ameelekeza kuhakikisha wakati wote wakiwapo wageni wenye ujuzi, nyuma yao wawapo Watanzania wanaojifunza hizo kazi na baada ya muda, utaalamu tubaki nao wenyewe," alisema.

Katambi alisema GGML imekuwa mfano wa kuigwa katika ununuzi unaofanyika kwenye migodi yake kwa sababu serikali kupitia mpango wa 'local content' inasisitiza vitu kama vipo nchini vinunuliwe nchini ili kuongeza ukwasi ndani ya nchi na kudhibiti fedha nyingi kwenda nje.

"Lakini pia mmezingatia usalama wa mazingira kwa ujumla ili tusipate watu wenye ulemavu unaotokana na migodi, pia mazingira na ardhi yetu inabaki kuwa salama," alipongeza.

Akimkaribisha katika banda hilo, meneja anayehusika na usalama kazini kutoka GGML, Isack Senya, alisema zaidi ya wananchi 3,000 wametembelea banda hilo na kujifunza mambo mbalimbali kuhusu teknolojia zinazotumika kufanya kazi katika mazingira yenye afya na usalama.

Alisema mwaka huu GGML ilileta vifaa vya kiteknolojia na kisasa kiasi cha kuiwezesha kampuni hiyo kuibuka kampuni bora yenye ubunifu kwenye vifaa hivyo.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu), Prof. Joyce Ndalichako, pia alipita katika banda hilo na kuipongeza kampuni hiyo kwa kuwa mdau muhimu katika kuzingatia matakwa ya sheria yanayosisitiza afya na usalama mahali pa kazi.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI**
**TAASISI YA TEKNOLOJIA YA UJENZI**

**TANGAZO LA KOZI YA UKARABATI NA MATENGENEZO YA BARABARA KWA KUTUMIA TEKNOLOJIA STAHIKI YA NGUVU KAZI 'LBT'**

**1. UTANGULIZI:**
Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi "Institute of Construction Technology(ICoT)" ni Chuo cha Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi chenye makao yake makuu Morogoro. Chuo kinawatangazia wananchi wote kuwa kinatarajia kuendesha kozi ya Ukarabati na Matengenezo ya Barabaraza Udongo/Changarawe kwa Wanawake na Vijana, na Kozi ya lami kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi katika Kampasi ya ICoT – Mbeya kama ifuatavyo: -

| | Jina la kozi | Muda wa Mafunzo | Mafunzo ya tafanyika |
|---|---|---|---|
| 1 | Kozi Maalumu ya Vikundi vya Wanawake na Vijana katika Ukarabati na Matengenzo ya barabara za changarawe/udongo (Gravel/Earth Roads) kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi. | **Wiki Nne (4)** 22/05/2023 – 17/06/2023 | **Mkoani Mbeya (ICoT – Mbeya)** |
| 2 | Kozi ya Lami (Surface Dressing for Low Traffic Volume Roads) kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi | **Wiki Nne (4)** 14/08/2023 - 09/09/2023 | **Mkoani Mbeya (ICoT – Mbeya)** |

**2. MASOMO YATAKAYOFUNDISHWA:**

(a) Kozi ya Ukarabati na Matengenezo ya Barabara za Changarawe/Udongo (Gravel/Earth Roads) kwa Kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi:
Kozi hii, Washiriki watajifunza maada mbalimbali juu ya ukarabati na matengenezo ya barabara za changarawe kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi pamoja na maada shirikishi ambazo ni; utaratibu wa kufungua kampuni, utaratibu wa kujaza kitabu cha zabuni, Teknolojia ya Udongo na Zege Ukarabati na Matengenezo ya barabara na Usimamizi sehemu ya kazi. Kipekee, kozi hii imelenga kumwezesha Wanawake na Vijana (washiriki) kupata ujuzi wa kufanya na kusimamia kazi za matengenezo ya barabara hasa matengenezo ya kawaida yaani 'Routine/Recurrent Maintenance'.

(b) Kozi ya Lami (Surface Dressing for Low Traffic Volume Roads) kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi:
Kozi hii, Washiriki watajifunza mada mbalimbali juu ya ujenzi wa barabara za lami (Surface Dressing for low Traffic Volume Roads) kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi pamoja na maada shirikishi ambazo ni: Maada juu ya vifaa na Mitambo midogo midogo, Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi na matengenezo ya barabara za lami.

**3. NJIA ZA UFUNDISHAJI**
Mafunzoyatafanyikakatikaawamumbili; awamuya kwanza itakuwanadharia (Darasani) naawamuyapiliitakuwanimafunzoyavitendo ('Site').

**4. MALENGO YA KOZI**
Masomo katika kozi hizi yamelenga kumpatia mshiriki mbinu mbalimbali juu ya matumizi ya Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi katika:

i. Kufanya na kusimamia kazi za matengenezo ya barabara hasa matengenezo ya kawaida yaani 'Routine/Recurrent, Periodic and Emergency maintenance';
ii. Kufanya na kusimamia kazi za ukarabati wa barabara yaani 'road rehabilitation';
iii. Kuendesha na kusimamia miradi ya matengenezo na ukarabati wa barabara za vumbi/changarawe na barabara za lami;
iv. Kwa wajasiriamali, masomo haya yatawawezesha kujiajiri kwa kufungua kampuni za ujenzi wa barabara zinazotumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi yaani **"SPECIALIST CIVIL WORKS-LABOUR BASED CONTRACTORING FIRMS"** kisha kupata sifa za kisheria za kununua kazi za miradi ya ujenzi au ukarabati wa barabara zinazotolewa na TARURA au TANROADS.

**5. WALENGWA WA MAFUNZO:**

a) Wahandisi wote wa barabara kutoka sekta ya Umma na binafsi,
b) Mafundi Sanifu wa barabara kutoka sekta ya Umma na binafsi,
c) Wasimamizi wa Miundombinu (Estates Managers) toka taasisi mbalimbali za Umma na Binafsi,
d) Makandarasi wenye nia ya kujenga au kuimarisha uwezo wa kazi zao za matengenezo/ ukarabati wa barabara kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi na,
e) Watu binafsi wenye uzoefu katika kazi za barabara au majengo na wanaohitaji kujiendeleza na kujifunza zaidi kazi za barabara.

**6. LUGHA YA MAFUNZO:**
Lugha itakayotumika katika Kozi ya Lami kwa Kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi ambayo itaendeshwa kwa muda wa wiki nne (4) ni Kiingereza; kozi ya ukarabati na matengenezo ya barabara ya changarawe/udongo maalumu ya vikundi vya wanawake na vijana itaendeshwa kwa kutumia mchanganyiko wa lugha ya Kiingereza na Kiswahili.

**7. ADA ZA USHIRIKI**

**a) Koziya Ukarabati na Matengenezo ya Barabara za Uhangarawe/Udongo kwa vikundi vya Wanawake na Vijana**
i. Mshiriki atakayepata huduma za chakula na malazi zinazotolewa na Chuo atalipa ada kiasi cha Tsh. 500,000.

**b) Kozi ya Lami (Surface Dressing for Low Traffic Volume Roads)**
i. Mshiriki atapata huduma za chakula na malazi zinazotolewa na Chuo atalipa ada kiasi cha Tsh. 1,000,000.00

Ada ya ushiriki zilipwe kwa kutumia **'Control Number'** itakayotolewa kwa mtu atakayehitaji mafunzo kwa kuwasiliana na uongozi mapema kabla yakozi kuanza. Inashauriwa kuwa ada ilipwe angalau wiki mbili kabla ya kozi kuanza.

**8. NAMNA YA KUTUMA MAOMBI YA KOZI:**

Wale wote watakaohitaji kujiunga na kozi yoyote kati ya hizi zilizotajwa hapo juu wanatakiwa kutuma maombi yao kwa kutumia anuani ya Posta au barua pepe zilizotolewa hapa chini au wanaweza kupiga simu kwa kutumia namba zilizotolewa kwa kupata maelezo zaidi.

**WASILIANA NASI**
**MKUU WA CHUO**
**TAASISI YA TEKNOLOJIA YA UJENZI (ICoT)**

| | |
|---|---|
| **S.L.P 963, MOROGORO**<br>**Simu : 023- 2935229/023- 2935226**<br>**: 0686 220 590 / 0759 077 606**<br>**: /0715 972 010**<br>**Nukushi : 023-2935227**<br>**Barua pepe : mwti@morogoro.net**<br>**Tovuti : www.icot.ac.tz** | **S.L.P 1957, MBEYA**<br>**Simu : 025 295 7484/5;**<br>**: 0764 775 354; 0769 317 404; 0765 251 509**<br>**Nukushi : 025 295 7486**<br>**Barua pepe : attimbeya@mow.go.tz**<br>**attimbeyafrica@gmail.com**<br>**Tovuti : www.icot.ac.tz** |

SIKU YA UHURU WA VYOMBO VYA HABARI

# Rais Dk. Samia, kada ya wanahabari wabadilishana pongezi na tabasamu

## •Wakiri wanachoomba amewawekea mezani

**Na Mwandishi Wetu**



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akizungumza na wanahabari mkutanoni Arusha. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

WAKATI leo kunafanyika sherehe za Siku ya Uhuru wa Habari, lililo bayana nchini kwa pande zote za Muungano, kunashuhudiwa unasaba wa moja kwa moja kitaaluma na kidemokrasia na sekta ya habari.

Kielelezo kinaaanzia na kinachojiri leo katika maadhimsho ya Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari kitaifa ikiwa mjini Unguja na mgeni rasmi ni Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi.

Hilo linafanyika visiwani, mchakato wa kupitia maoni ya mabadiliko ya sheria inayohusu habari ikiwa katika ngazi ya mapitio ya ndani ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) na bara, muswada umeshasomwa kwa mara ya kwanza bungeni mwaka huu.

Ikibaki katika picha ya Muungano, pia iko bayana zaidi pale Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, anaishi na kutabasamu na kada ya wanahabari, anawapata kwa majina akiwataja na kama kawaida yake akiwachomekea masihara ya kindugu kuwafahamu vijana wake wa kitaifa na hajawa mvivu wanapomwomba kwenye lao.

Tangu mwanzo wa utawala wake kushika uongozi wa nchi, miongoni mwa yaliyoanza katika zama hizo Watanzania wakisikia mengi ya kuamuliwa yanayobeba ahueni, pia neema ambayo nayo si haba kwa wanahabari, 'kufumba na kufumbua' uhuru wao kitaaluma ukawafikia, ujumbe ukipitia kwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye.

Nafasi ya ushuhuda dhahiri ukawa pale mwanzoni mwa Februari mwaka jana, serikali ilipoyafungulia magazeti kama Mwanahalisi, Mawio, Mseto na Tanzania Daima pasipo masharti yoyote, ambayo yalikuwa yamefungiwa tangu zama 2020. Ni hatua iliyopokewa kwa shangwe kuanzia wanahabari na wapenda haki mbalimbali wa kitaaluma na wasio wa kitaaluma.

Ni mambo yanayoendana na salamu rasmi za kiserikali kupitia kwa waziri mwenye dhamana, Nape Nnauye, akiwataka kuandika habari kwa uhuru, ili mradi wachunge lugha zao.

Hilo akalirejea tena wakati akitimiza mwaka mmoja wa kuwapo madarakani, Waziri Nape akiwasilisha salamu za Rais, akivipongeza vyombo vya habari nchini kutokana na kufanya kazi nzuri mwaka mmoja kuwapo kwake madarakani,vikiandika habari ambazo hazikuligawa taifa, wala kuleta chuki.

"Rais Samia anavishukuru vyombo vya habari kwa kazi nzuri katika mwaka 2022 ya kuandika habari za kuhabarisha, kuelimisha na kuburudisha na kubwa kuliko yote ni kuunganisha taifa," akatamka Nape wakati anazungumza na waandishi wa habari Machi mnamo mwaka jana, Rais Dk. Samia alipotimiza mwaka mmoja.

"Rais Dk. Samia anawasalimia sana. Ameniambia, niwaambie mfanye kazi bila woga, bila upendeleo wala uonevu huku mkizingatia taaluma," akatamka, akiambatanisha na ufafanuzi kwamba Rais ni muumini wa haki ya kujieleza na kutoa maoni, hivyo haoni sababu ya kuminya uhuru wa habari.

**RAIS MKUTANONI**

Hata ilipofika Mei ya mwaka 2022, ni mara nyingine Rais Dk. Samia akawa mgeni Rasmi meza moja katika maadhimisho kama ya leo Zanzibar ya mwaka jana yakiwa mkoani Arusha, ambako akawataka watumiaji mitandao ya kijamii, pamoja na waandishi wa habari Afrika, kuelekeza taaluma zao kuandika mazuri ya bara hilo yanayojumuisha utajiri wa rasilimali, uzuri wake, mila na desturi ili kulinda hadhi ya nchi zao, wakizingatia miko yao kitaaluma.

Ni sherehe iliyohudhuriwa na wajumbe wastani 400, wakiwamo wanaotoka nchi sita za Afrika Mashariki; Rwanda, Sudani Kusini, Ethiopia, Kenya, Uganda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Ni aina ya maadhimisho yaliyopokewa na mwitikio wa bashasha kutoka kwa wenye taaluma yao na wenyeji wa hafla, waandishi wa habari na wenyeji wa sekta hiyo. Hapo pia ikaangukia hatua nyingine ya tabasamu, kuhusu gharama za usajili wa mitandao ya habari.

Mahsusi ni pale Rais Dk. Samia akamwagiza Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye kushughulikia maombi ya uwezekano wa kuondolewa au kupunguzwa kodi na ushuru wa forodha na ongezeko la thamani kwa karatasi za kuchapisha magazeti, ikiwa ni mojawapo ya maombi yaliyotolewa na Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF).

Ni hatua ambayo leo, Mwenyekiti wa Jukwaa la Misa- Tan, Salome Kitomari, anakiri baada ya mwaka mmoja, kuna viashiria vyema kwa vyombo vingi vya vyombo vya habari vya mtandaoni viko huru na vinaongezeka, huku hatua hiyo ikifanyiwa kazi ya gharama na mamlaka husika.

Katika hotuba ya kumkaribisha mgeni, Rais Dk. Samia, Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Deodatus Balile, akaipongeza serikali kuendelea kuitambua tasnia ya habari na kwa mara ya kwanza kupokea Muswada wa Sheria ya Huduma ya Habari wenye maoni ya mabadiliko.

"Tunamshukuru Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kutufungulia njia... tangu aingie madarakani amebadilisha upepo na kuweka mazingira mazuri ya mawasiliano kati ya vyombo vya habari na serikali," akatamka Balile.

Pia, akasema wakati huo (mwaka jana) unafuu uliowekwa na serikali, bado vyombo vya habari havipo vizuri kiuchumi, hata vilivyofunguliwa vimeshindwa kuendesha huduma hiyo kutokana na uchumi mdogo.

Hata hivyo, inaelezwa kuna sehemu ya hatua zimechukuliwa na serikali hadi sasa, ikiwa ni utekelezaji wa ombi la wanahabari, serikali kuendelea kulipa lindi la madeni kwa yaliyokuwapo awali.

**MSIMAMO WA RAIS**

Katika Mkutano wa Waziri Nape na wanahabari miezi michache kabla maadhimisho ya Arusha mwaka jana, akawafikishia ujumbe Rais Dk. Samia kuhusu msimamo, akitamka: "Rais alishawahi kuniambia wakati wa mchakato ya kupitia Sheria ya Habari kuwa tuhakikishe hatuingilii haki ya watu kujieleza. Nasi tumekuwa tukilifanya hilo, niwaombe kwa pamoja tutafsiri maono ya rais wetu, yeye nia na dhamira yake ni kuona uhuru wa habari unaleta tija kwa nchi."

Hadi sasa muswada wa sheria hiyo umeshasomwa bungeni kwa mara ya kwanza. Pia, Waziri Nape akafafanua msimamo wa kiserikali akiwataka waandishi wa habari kuendelea kuandika habari za uchunguzi, ili kuibua changamoto zilizopo kwenye jamiii, kusaidia serikali kutekeleza majukumu yake. Kuhusu madeni inayodaiwa serikali na vyombo vya habari.

Vilevile Nape, akafafanua kuhusu mchakato wa kulipa madeni ya serikali kwa vyombo vya habari, wakati huo Machi mwaka jana yakiwa zaidi ya shilingi bilioni 18. Kwa taarifa zilizopo ni kwamba, vyombo mbalimbali vya habari sasa, vimeshaanza kulipwa pesa zao.

Inatajwa katika historia ya habari nchini, Nape anayetumikia Wizara ya Habari katika serikali ya Awamu ya Sita, ndiye pekee waziri aliyepewa tuzo ya heshima tangu uhuru wa nchi.




Wanahabari wakimsikiliza Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, katika mkutano mkoani Arusha mwaka jana.

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

**Wizara ya Mifugo na Uvuvi**

# HOTUBA YA MHESHIMIWA ABDALLAH HAMIS ULEGA (MB) WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI, AKIWASILISHA BUNGENI MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI KWA MWAKA 2023/2024



Mhe Abdallah Hamis Ulega (Mb), Waziri wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi



Mhe David Ernest Silinde (Mb), Naibu Waziri wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi



Dkt. Daniel Elius Mushi, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Mifugo)



Prof. Riziki Silas Shemdoe, Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi



Bibi Agnes Kisaka Meena, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi)

## BAJETI YA MIFUGO NA UVUVI 2023/2024

# SEKTA YA MIFUGO
# UFUGAJI WENYE TIJA

1. Kuongeza Malisho ya Mifugo
2. Kuongeza Soko la Biashara ya Nyama
3. Kuchochea Ufugaji wa Kisasa
4. Kuongeza Fursa za Ajira na Kipato Kwenye Mnyororo wa Thamani wa Sekta ya Mifugo
5. Kuongeza Mchango wa Ufugaji Kwenye Pato la Taifa

#MifugoNaUvuviNiUtajiri

## BAJETI YA MIFUGO NA UVUVI 2023/2024

# SEKTA YA UVUVI
# UCHUMI WA BULUU

1. Kusudio la Kuanzisha Mamlaka ya Uvuvi
2. Kuwawezesha Wavuvi Kupata Boti za Kuvua Kwenye Kina Kirefu
3. Kutoa Mikopo Isiyo na Riba kwa Wavuvi Wadogo
4. Kuongeza Ufugaji wa Samaki Kukidhi Mahitaji
5. Kuongeza Fursa za Ajira na Kipato Kwenye Mnyororo wa Thamani wa Sekta ya Uvuvi
6. Kuongeza Mchango wa Uvuvi Kwenye Pato la Taifa

*#MifugoNaUvuviNiUtajiri*





# HOTUBA YA MHESHIMIWA ABDALLAH HAMIS ULEGA (MB) WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI KWA MWAKA 2023/2024

**A. UTANGULIZI**

1. ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo iliyochambua Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Fungu 99 – Mifugo na Fungu 64 – Uvuvi); Naomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee, lijadili na kupitisha taarifa ya utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka 2022/2023 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya mwaka 2023/2024 kwa Fungu 99 – Mifugo na Fungu 64 – Uvuvi.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha hotuba yangu ya kwanza siku ya leo. Aidha, kwa namna ya pekee napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi na kumteua **Mhe. David Ernest Silinde** (Mb) kuwa Naibu Waziri, tunaahidi kutumia uwezo wetu wote kutekeleza wajibu wetu kwa ufanisi na uadilifu na kuhakikisha rasilimali za mifugo na uvuvi zinasimamiwa na kutumika kikamilifu ili kuchangia mapinduzi ya uchumi wa nchi yetu.

3. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda pia kutumia nafasi hii kumpongeza **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa umahiri wake mkubwa anaouonesha katika kuiongoza nchi yetu na kuifanya iendelee kupiga hatua kubwa za maendeleo ya kiuchumi, kijamii, kisiasa na kuaminika Kimataifa. Pia nimpongeze **Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango**, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna anavyoshirikiana na Mheshimiwa Rais kuwaletea maendeleo watanzania. Wizara ya Mifugo na Uvuvi tunaahidi kuendelea kuwaunga mkono na kutekeleza dira, miongozo na maelekezo wanayoyatoa katika kuwatumikia wananchi hususan wafugaji, wavuvi, wachakataji, wasindikaji na wafanyabiashara wa mifugo na samaki na mazao yake kwa maslahi mapana ya nchi yetu. Nitumie nafasi hii kuwaombea viongozi wetu kwa Mwenyezi Mungu, wawe na afya njema, na aendelee kuwapa hekima na busara katika kuiongoza nchi yetu. Vilevile, nampongeza **Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi**, Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuendelea na usimamizi mahiri wa shughuli za maendeleo katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

4. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutumia nafasi hii kumpongeza **Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb),** Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mbunge wa Jimbo la Ruangwa kwa kazi nzuri ya uratibu na usimamizi wa shughuli za Serikali. Pia, namshukuru na kumpongeza, kwa hotuba yake nzuri ambayo imebainisha malengo na kazi zitakazotekelezwa na Serikali kwa mwaka 2023/2024. Wizara ya Mifugo na Uvuvi ipo tayari kutekeleza malengo hayo ili kuwaletea maendeleo wananchi na kukuza uchumi wa Taifa letu.

5. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kukupongeza wewe binafsi na ***Mheshimiwa* Naibu Spika**, kwa kuendelea kuliongoza Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ni wazi kuwa chini ya uongozi wenu Bunge letu la 12 limeendelea kuwa mahiri zaidi katika kuisimamia na kuishauri Serikali na hivyo kuongeza ufanisi katika kusimamia rasilimali za umma na kuwatumikia wananchi. Aidha, napenda kuwapongeza Wenyeviti wa Kamati mbalimbali za Bunge kwa kuteuliwa kuongoza Kamati hizo.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya pekee napenda kumpongeza Mhe**. David Mwakiposa Kihenzile (Mb)** kwa kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, **Mhe. Mariam Ditopile Mzuzuri (Mb)** kuwa Makamu Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge wote walioteuliwa kuwa Wajumbe wa Kamati, tunaahidi kuwapa ushirikiano katika kutekeleza majukumu yao ya usimamizi wa Sekta za Mifugo na Uvuvi. Pia, natoa shukran za dhati kwa Kamati kwa maelekezo na ushauri wao mzuri walioutoa wakati wa kupitia Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2022/2023 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa mwaka 2023/2024. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Wizara yangu itaendelea kuzingatia ushauri, mapendekezo na maoni ya Kamati na yale yatakayotolewa na Bunge lako Tukufu.

7. ***Mheshimiwa Spika,*** namshukuru Katibu Mkuu wa Wizara **Prof. Riziki Silas Shemdoe** na Naibu Makatibu Wakuu **Dkt. Daniel Elius Mushi** (Mifugo) na **Bi. Agnes Kisaka Meena** (Uvuvi) kwa kuwa viungo muhimu kati yangu na watumishi na kuniwezesha kutekeleza majukumu ya Wizara kwa ufanisi. Kipekee, ninawashukuru kwa dhati na kuwapongeza watumishi wote wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kazi nzuri wanayofanya katika kuendeleza Sekta za Mifugo na Uvuvi nchini.

8. ***Mheshimiwa Spika***, naomba kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Mkuranga, kwa ushirikiano wanaoendelea kunipa katika kuwawakilisha na kuwatumikia katika Bunge hili Tukufu pamoja na kutekeleza shughuli mbalimbali za maendeleo katika Jimbo.

9. ***Mheshimiwa Spika***, kwa namna ya kipekee napenda kuishukuru familia yangu hususan Mke wangu kipenzi Bi. Mariam Abdallah Ibrahim na watoto wangu kwa kunivumilia na kunitia moyo katika utekelezaji wa majukumu yangu.

10. ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya maelezo ya utangulizi, naomba sasa kuwasilisha taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2022/2023 na Mpango wa Bajeti ya Wizara wa Mwaka 2023/2024 kwa Fungu 99 - Mifugo na Fungu 64 – Uvuvi ambayo pia inapatikana katika vishikwambi vya Waheshimiwa Wabunge na Tovuti ya Wizara: www.mifugouvuvi.go.tz.

**B. SEKTA YA MIFUGO (FUNGU 99)**

**UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2022/2023**

**Maeneo ya Kipaumbele katika Mwaka 2022/2023**

11. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023 Wizara ilianza kutekeleza Mpango wa Mabadiliko ya Sekta ya Mifugo ili kuchangia ipasavyo katika ukuaji wa uchumi na Pato la Taifa, na kupunguza umaskini. Maeneo ya kipaumbele yaliyozingatiwa yalikuwa: **kuimarisha huduma za maji, malisho na vyakula vya mifugo; kuwezesha upatikanaji wa mbegu bora za mifugo; kuimarisha afya ya mifugo; kuboresha huduma za ugani; kuimarisha huduma za utafiti na mafunzo ya taaluma za mifugo; kuimarisha masoko; na kuwezesha uongezaji thamani mazao ya mifugo**.

**Makusanyo ya Maduhuli**

12. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023 Wizara kupitia Fungu 99 ilitarajia kukusanya kiasi cha shilingi **bilioni 40.1**. Hadi kufikia tarehe 30 Machi, 2023 kiasi cha shilingi **bilioni 19.9** kimekusanywa.

**Fedha zilizoidhinishwa kwa Ajili ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo 2022/2023**

13. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya Wizara kupitia Fungu **99** ilikuwa Shilingi **bilioni 92.0**, ambapo kati ya fedha hizo Shilingi **bilioni 21.3** zilikuwa ni mishahara, Shilingi **bilioni 24.0** matumizi mengineyo (OC) na Shilingi **bilioni 46.7** kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo, ikijumuisha Shilingi **milioni 138.9** fedha za nje kwa ajili ya miradi.

**Matumizi ya Bajeti ya Kawaida na Maendeleo**

14. ***Mheshimiwa Spika,*** Hadi Machi 31, 2023 Shilingi **bilioni 29.6** zimepokelewa na kutumika kwa ajili ya matumizi ya kawaida, sawa na **asilimia 65.4** ya Shilingi **bilioni 45.3** zilizotengwa. Kati ya fedha hizo, Shilingi **bilioni 15.4** zimetumika kulipa Mishahara na Shilingi **bilioni 14.2** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC).

15. ***Mheshimiwa Spika,*** Shilingi **bilioni 27.2** sawa na asilimia **58.4** ya Shilingi **bilioni 46.7** zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo zimepokelewa na kutumika hadi Machi 31, 2023. Kati ya fedha hizo, Shilingi **bilioni 27.1** ni fedha za ndani na Shilingi **milioni 106.9** ni fedha za nje.

**Hali ya Sekta ya Mifugo**

16. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, idadi ya mifugo nchini imeongezeka kutoka ng'ombe **milioni 35.3** hadi ng'ombe **milioni 36.6**, mbuzi kutoka **milioni 25.6** hadi **milioni 26.6** na kondoo kutoka **milioni 8.5** hadi **milioni 9.1.** Pia, kuku wameongezeka kutoka **milioni 92.8** hadi **milioni 97.9** ambapo kuku wa asili wameongezeka kutoka **milioni 42.7** hadi **milioni 45.1,** kuku wa kisasa kutoka **milioni 50.1** hadi **milioni 52.8** na nguruwe kutoka **milioni 3.4** hadi **milioni 3.7.** Aidha, ukuaji wa Sekta ya Mifugo kwa mwaka 2021 umefikia **asilimia 5.0** na kuchangia **asilimia 7.0** kwenye Pato la Taifa.

17. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023 ng'ombe **2,218,293** na mbuzi/kondoo **2,121,187** wenye thamani ya Shilingi **trilioni 1.7** waliuzwa katika minada mbalimbali hapa nchini ikilinganishwa na ng'ombe **2,194,937**; mbuzi/kondoo **1,782,010** wenye thamani ya Shilingi **trilioni 1.5** waliouzwa katika mwaka 2021/2022.

18. ***Mheshimiwa Spika,*** uzalishaji wa nyama umeongezeka kwa asilimia **4.3** kutoka tani **769,966.7** mwaka 2021/2022 hadi tani **803,264.3** mwaka 2022/2023. Uzalishaji wa maziwa umeongezeka kutoka lita **bilioni 3.4** mwaka 2021/2022 hadi kufikia lita **bilioni 3.6** mwaka 2022/2023 sawa na ongezeko la asilimia **5**. Vipande vya ngozi **milioni 14.1** vimezalishwa mwaka 2022/2023 ikilinganishwa na vipande **milioni 13.6** vilivyozalishwa mwaka 2021/2022. Uzalishaji wa mayai umeongezeka kutoka mayai **bilioni 4.9** mwaka 2021/2022 hadi **bilioni 5.5** mwaka 2022/2023 sawa na ongezeko la asilimia **12.2.**

19. ***Mheshimiwa Spika,*** asilimia ***35*** ya kaya zilizopo nchini zinajishughulisha na ufugaji, kati ya hizo asilimia **39.3** wanafuga ng'ombe, asilimia **36.2** wanafuga mbuzi, asilimia **13.5** wanafuga kondoo na asilimia **10.9** wanafuga nguruwe. Aidha, asilimia **55.4** ya kaya hizo pia hujishughulisha na ufugaji wa kuku.

**Utekelezaji wa Majukumu ya Sekta ya Mifugo**

***Sera, Sheria na Kanuni***

20. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Wizara imekamilisha mapitio ya Sera ya Taifa ya Mifugo ya Mwaka 2006 na kuandaa rasimu. Aidha, Sheria tisa (**9**) za Sekta ya Mifugo zimefanyiwa urekebu (revision*)* ambapo zinasubiri kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali. Vilevile, Marekebisho yamefanyika kwa kanuni mbili (**2**) zilizo chini ya Sheria ya Magonjwa ya Wanyama SURA 156 pamoja na Sheria ya Tasnia ya Nyama SURA 421 na tafsiri ya kanuni mbili (**2**) imefanyika kutoka katika lugha ya Kiingereza kwenda lugha ya Kiswahili. Aidha, Wizara imetangaza notisi ya wakaguzi wa Ngozi **101** yenye GN No.285/2023 kupitia Sheria ya Biashara ya Ngozi SURA 120.

***Maji, Malisho na Vyakula vya Mifugo***

21. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Wizara kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI imetambua na kuyasajili maeneo **77** ya malisho yenye jumla ya hekta **994,827.29** kutoka kwenye Halmashauri **8** za Wilaya, ambapo maeneo hayo yametangazwa kwenye Gazeti la Serikali kwa G.N **597** ya tarehe 7/10/2022. Pia, Wizara kwa kushirikiana na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi imetenga jumla ya hekta **195,028.29** za maeneo ya malisho katika Halmashauri za Wilaya **14** na hivyo kufanya maeneo ya malisho yaliyotengwa kufikia hekta **3,384,485.54** kutoka hekta **3,189,456.94** mwaka 2021/2022, sawa na ongezeko la **asilimia 6.1**.

22. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, kilo **22,691.65** za mbegu bora za malisho zimezalishwa ikilinganishwa na kilo **4,481.90** zilizozalishwa mwaka 2021/2022. Pia, marobota **248,209** ya hei yamevunwa katika mashamba ya Serikali na binafsi. Aidha, taarifa kuhusu ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya maji kwa ajili ya mifugo inapatikana katiba ibara ya **64** ya Hotuba yangu.

23. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali za Mitaa imeanzisha mashamba darasa **100** ya malisho yenye ukubwa wa ekari **520** katika Halmashauri **44** na kusambaza mbegu tani **8.56** kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa na wafugaji binafsi.

***Kuendeleza Ufugaji Kijiji cha Msomera***

24. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuendeleza eneo la wafugaji la Msomera, Wizara imetekeleza yafuatayo:- kupima na kutenga vitalu vya ufugaji **112** vyenye ukubwa wa hekta **100** kila kimoja kwa ajili ya malisho; kujenga bwawa la maji, kujenga majosho sita (**6**) na kukarabati moja (**1**); kuhimilisha ng'ombe **1,252**; kuanzisha mashamba darasa manne (**4**) yenye ukubwa wa ekari **10** kila moja na kuyapatia mbegu za malisho kilo **280**; kusambaza mbegu za malisho kilo **110** kwa wafugaji binafsi; na kusaidia uhamishaji wa mifugo **13,937** kutoka Pori Tengefu la Loliondo kwenda Msomera. Aidha, kwa kushirikiana na Heifer International, wananchi wamehamasishwa kuunda ushirika wa wafugaji, wamefundishwa usindikaji mdogo na biashara ya maziwa.

***Uzalishaji Mbegu Bora na Masoko***

25. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Wizara imezalisha dozi **116,558** za mbegu bora za ng'ombe katika Kituo cha Taifa cha Uhimilishaji (NAIC). Pia, ng'ombe **60,697** wamehimilishwa nchini ikilinganishwa na ng'ombe **64,463** waliohimilishwa mwaka 2021/2022. Aidha, madume bora **366** ya ng'ombe yamenunuliwa na kusambazwa kwa vikundi vya Wafugaji.

26. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Wizara imejenga minada **19** na kukarabati minada minne (**4**) ili kuboresha mazingira ya biashara ya mifugo. Pia, mizani **82** imenunuliwa na inaendelea kusambazwa kwenye minada.

***Afya ya Mifugo***

27. ***Mheshimiwa Spika,*** Hadi Oktoba 30, 2022, jumla ya mifugo **5,292,738** wametambuliwa na kusajiliwa kwenye mfumo wa utambuzi.

28. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, lita **52,560** za dawa za kuogesha mifugo zenye thamani ya shilingi **bilioni 2.39** zimenunuliwa na kusambazwa. Aidha, ujenzi wa majosho **257** katika Mamlaka **83** za Serikali za Mitaa unaendelea.

29. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, jumla ya dozi **243,365,631** za chanjo zimetolewa kwa mifugo mbalimbali dhidi ya magonjwa mbalimbali ikilinganishwa na dozi **223,592,415** zilizotolewa mwaka 2021/2022.

**Ugani, Utafiti na Mafunzo**

***Huduma za Ugani wa Mifugo***

30. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023, Wizara imenunua Pikipiki **1,200** kwa ajili ya Maafisa Ugani na magari **13** kwa ajili ya kuratibu huduma za ugani katika Sekretarieti za Mikoa. Pia yametolewa mafunzo rejea kwa maafisa ugani **515.** Aidha, maafisa ugani **3,018** kati ya **3,201** wamesajiliwa katika mfumo wa M- Kilimo.

**Uratibu wa Utafiti na Mafunzo ya Mifugo**

31. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023, Wizara imeanzisha vituo atamizi nane (**8**) vyenye uwezo wa kuwa na vijana **240** kwa wakati mmoja. Hadi kufikia mwezi Machi, 2023 jumla ya vijana **238** wakiwemo wa kike **71** na wa kiume **167** wamesajiliwa. Vijana hao wamewezeshwa kununua jumla ya ng'ombe **2,222** (ikiwa sehemu ya mafunzo) kwa ajili ya utekelezaji wa mpango huo ambapo kila mnufaika anapatiwa ng'ombe **10** wa kunenepesha na kuwauza kila baada ya miezi mitatu kwa awamu nne kwa mwaka hadi anapohitimu.

**Taasisi Zilizo Chini ya Sekta ya Mifugo**

***Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO)***

32. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuimarisha utendaji wa NARCO, Wizara imeanza kutekeleza Mpango wa mabadiliko wa miaka mitatu (2022/2023 hadi 2024/2025) wenye vipengele vitano ambavyo ni:- uboreshaji wa Mbari za Mifugo; uendelezaji wa malisho na vyakula vya mifugo; unenepeshaji wa mifugo; skimu za unenepeshaji kupitia vijana na wanawake; na uendelezaji wa masoko. Aidha, utekelezaji wa maeneo hayo umehusisha uwekezaji wa shilingi **bilioni 4.6** zilizotengwa kutoka

Serikalini zilizowezesha kununua ng'ombe wazazi **1,000**, matrekta manne (**4**), Tela nne (**4**), Beila tatu (**3**), Reki moja (**1**) na kuchimba visima virefu **7** katika ranchi za Kongwa, Mzeri na Ruvu. Uwekezaji huu utaiwezesha NARCO kutumia maeneo yake kikamilifu na kuongeza tija. Aidha, katika mwaka 2022/2023, marobota **38,200** ya malisho yamezalishwa na nyama (*kongwa beef*) tani **159.2** zimezalishwa na kuuzwa.

***Bodi ya Nyama Tanzania***

33. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Wizara kupitia Bodi ya Nyama, imeendelea kusimamia biashara ya nyama kwenda nje ya nchi, ambapo hadi Aprili 30, 2023 tani **12,243.79** zenye thamani ya Dola za Marekani **51,894,622.44** zimeuzwa nje ya nchi ikilinganishwa na tani **8,877.80** zenye thamani ya Dola za Marekani **36,264,786.13** kwa kipindi kama hicho mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia **43.1**. Biashara imekua kutokana na jitihada za **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuboresha mazingira ya biashara na kuvutia uwekezaji, pamoja na uwepo wa machinjio sita (**6**) zenye ithibati ya kusafirisha nyama nje ya nchi.

**Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania**

34. ***Mheshimiwa Spika,*** Hadi Machi 31, 2023 Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania (TVLA) imezalisha dozi **51,034,610** za aina saba (**7**) za chanjo za magonjwa ya kipaumbele na kuzisambaza nchini ikilinganishwa na dozi **50,640,250** zilizozalishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2022.

**Wakala ya Mafunzo ya Mifugo (LITA)**

35. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, LITA imeboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa kujenga kumbi nne (**4**) za Mihadhara na hosteli mbili (**2**) katika kampasi zake.

**MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2023/2024**

**Ukusanyaji wa Maduhuli**

36. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Wizara kwa upande wa Sekta ya Mifugo (**Fungu 99**) inatarajia kukusanya jumla ya Shilingi **42,105,000,000** kutoka kwenye vyanzo mbalimbali.

**Maeneo ya kipaumbele katika Sekta ya Mifugo**

37. ***Mheshimiwa Spika***, Mpango na Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Sekta ya Mifugo) kwa mwaka 2023/2024 umeandaliwa kwa kuzingatia vipaumbele vifuatavyo:-
    (i) Kuongeza uzalishaji na upatikanaji wa malisho na maji kwa ajili ya mifugo;
    (ii) Kuongeza ajira kwa vijana na wanawake ili kuimarisha upatikanaji wa malighafi za viwanda vya mazao ya mifugo;
    (iii) Kuboresha mbari za mifugo;
    (iv) Kuimarisha afya ya mifugo;
    (v) Kuboresha huduma za ugani, mafunzo na utafiti wa mifugo;
    (vi) Kuanzisha Mamlaka ya Kusimamia Miundombinu ya Mifugo; na
    (vii) Kuimarisha biashara na kuongeza thamani ya mifugo na mazao yake.

38. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kutekeleza vipaumbele hivyo, baadhi ya kazi zitakazofanyika katika mwaka 2023/2024 ni pamoja na:-

    (i) Kuanzisha skimu za umwagiliaji katika mashamba ya malisho ya Vikuge na Langwira, pamoja na ranchi za NARCO za Kongwa na Mzeri; Kujenga mabwawa na visima virefu kwa ajili ya maji ya mifugo; na kuanzisha mashamba darasa 150 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi za Wizara;

    (ii) Kuanzisha vituo vipya vya uwekezaji vya vijana na kuendeleza vituo vingine vilivyoanzishwa;

    (iii) Kuhimilisha ng'ombe 100,000; kuendelea kununua madume bora na kuyagawa kwenye vikundi vya wafugaji; kununua ng'ombe wazazi 1,200 kwa ajili ya mashamba ya Serikali ya kuzalisha Mitamba; na kuzalisha dozi 1,500,000 za mbegu bora za mifugo katika kituo cha NAIC;

    (iv) Kuendesha kampeni ya udhibiti magonjwa kwa kujenga majosho 246, kununua dawa za kuogesha mifugo lita 56,000 na kusambaza chanjo dozi 500,000,000;

    (v) Kununua pikipiki 1,200 na magari 3, zana za huduma za veterinari (vet kit) 1,100 na zana za uhimilishaji (AI Kit) 184; kuanzisha kampasi mpya ya LITA Songwe; kukamilisha taratibu za upatikanaji wa ithibati kwa mbegu za malisho ili ziuzwe madukani; na kuanzisha kituo cha utafiti wa mifugo cha Kanda ya Magharibi Wilayani Nsimbo mkoa wa Katavi;

    (vi) Kuanzisha skimu za unenepeshaji katika Mashamba ya NARCO na Vituo vya kupumzishia mifugo; Kujenga na kukarabati minada; na kufunga mizani kwenye minada 70 ya awali; na kujenga vituo 10 vya kukusanya maziwa;

    (vii) Kuiwezesha NARCO kuzalisha ndama 5,479 kutokana na majike wazazi 6,849 na kunenepesha ng'ombe 12,696 kupitia programu ya kujenga uwezo wa uwekezaji kwa vijana itakayofanyika katika ranchi ya NARCO Kongwa na kuzalisha marobota ya hei 55,000 katika ranchi ya Kongwa na Mzeri kwenye eneo la Ha.11,000;

    (viii) Kukusanya maoni ya wadau na kufanya tathmini ya uanzishaji wa Mamlaka ya Kusimamia na Kuendeleza Miundombinu ya Mifugo;

    (ix) Kuvutia wawekezaji kwenye mbegu bora za kuku, vyakula vya mifugo, madawa na chanjo, pamoja na uzalishaji wa mbari za mifugo na mbegu za malisho; na

    (x) Kutambua na kusajili kwenye mfumo wa kielektroniki takriban mifugo 40,603,262, ili kuwa na taarifa sahihi kwa ajili ya kuboresha mifugo na kukidhi hitaji la masoko.

**C. SEKTA YA UVUVI (FUNGU 64)**

**Hali ya Sekta ya Uvuvi**

39. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022, Sekta ya Uvuvi ilichangia asilimia **1.8** kwenye Pato la Taifa na kukua kwa asilimia **2.5**. Aidha, Sekta ya Uvuvi inatoa ajira za moja kwa moja kwa wavuvi **197,763** na wakuzaji viumbe maji **34,057** na takriban watanzania **Milioni 4.5** wanajishughulisha na shughuli mbalimbali zinazohusiana na uvuvi.

40. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, biashara ya mazao ya uvuvi imeendelea kuimarika katika soko la ndani na nje ya nchi. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2023, jumla ya tani **29,466.98** za mazao ya uvuvi zenye thamani ya Shilingi **bilioni 453.8** na idadi ya samaki hai wa mapambo **150,308** wenye thamani ya Shilingi **bilioni 1.82** waliuzwa nje ya nchi.

41. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, idadi ya miundombinu ya ukuzaji viumbe maji imefikia mabwawa **32,878**, vizimba **993,** vitotoleshi **39** vya kuzalisha vifaranga na viwanda nane (**8**) vya kutengeneza chakula cha samaki. Aidha, uzalishaji wa mazao mbalimbali ya ukuzaji viumbe maji ulifikia tani **33,525.5** na vifaranga vya samaki **35,967,180** ambapo kati ya hivyo, vifaranga **31,000** vimepandikizwa katika malambo mbalimbali nchini ili kuongeza upatikanaji wa samaki.

**MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2022/2023**

**Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka 2022/2023**

42. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara ilipanga kukusanya Shilingi **bilioni 40** kupitia Fungu 64. Aidha, jumla ya Shilingi **bilioni 17.4** zimekusanywa.

**Fedha zilizoidhinishwa kwa Mwaka 2022/2023**

43. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023, Wizara kupitia Fungu 64 ilitengewa jumla ya **Shilingi bilioni 176.2.** Kati ya fedha hizo, Shilingi **bilioni 40.5** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **bilioni 135.7** ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

**Matumizi ya Bajeti ya Kawaida**

44. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Fungu 64 lilitengewa jumla ya Shilingi **bilioni 40.5**. Kati ya fedha hizo, Shilingi **bilioni 12.7** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Wizara (PE) na Shilingi **bilioni 27.8** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC). Hadi Machi, 2023, jumla ya Shilingi **bilioni 16.8** zimetolewa, sawa na asilimia **41.5**





kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo Shilingi **bilioni 9.3** ni fedha za mishahara ya watumishi (PE) na Shilingi **bilioni 7.5** ni fedha za Matumizi Mengineyo (OC).

**Matumizi ya Bajeti ya Maendeleo**

45. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023, Wizara kupitia Fungu 64 ilitengewa kiasi cha Shilingi **bilioni 135.7** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ikiwa ni fedha za ndani na nje. Hadi Aprili, 2023, jumla ya maombi ya Shilingi **bilioni 41.2** yamewasilishwa ambapo kiasi cha Shilingi **bilioni 6.6** zimelipwa na Shilingi **bilioni 34.6** zipo kwenye hatua mbalimbali za malipo.

**UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU KATIKA MWAKA 2022/2023**

**Usimamizi na Udhibiti wa Rasilimali za Uvuvi**

46. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha usimamizi wa rasilimali za uvuvi, hadi kufikia Aprili, 2023, jumla ya siku kazi **4,743** za doria zimefanyika ambazo ni sawa na asilimia **60.8** ya lengo la mwaka.

**Uthibiti wa Ubora na Usalama wa Mazao ya Uvuvi**

47. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023, Wizara imefanya kaguzi **8,649** kati ya kaguzi **9,472** zilizopangwa ili kuhakiki ubora, usalama wa mazao ya uvuvi na uimara wa mfumo wa uzalishaji.

**Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu**

48. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Aprili, 2023 watalii **35,562** walitembelea Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu ambapo Shilingi **bilioni 1.68** zilikusanywa ikilinganishwa na watalii **22,562** na Shilingi **bilioni 1.18** zilizokusanywa mwaka 2021/2022 ikiwa ni ongezeko la asilimia **42.4**.

49. ***Mheshimiwa Spika,*** ongezeko hili la watalii limetokana na jitihada za **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuutangaza utalii kupitia filamu ya *The Royal Tour.*

**Ukuzaji Viumbe Maji**

50. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, jumla ya vifaranga **35,967,180** vya samaki vimezalishwa nchini ikilinganishwa na vifaranga **30,332,528** vya mwaka 2021/2022, sawa na ongezeko la asilimia **18.6** la uzalishaji. Vilevile, jumla ya wananchi **8,788** walipatiwa mafunzo kuhusu mbinu bora za ufugaji samaki na udhibiti wa magonjwa ikilinganishwa na wananchi **7,884** wa mwaka 2021/2022.

**Huduma za Ugani wa Uvuvi**

51. ***Mheshimiwa spika,*** katika mwaka 2022/2023, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu inaendesha programu ya atamizi maalum ya uvuvi na ukuzaji viumbe maji kwa vijana **500,** ambapo awamu ya kwanza imenufaisha vijana **200**. Vilevile, Wizara inaendelea na taratibu za kuwapata vijana wengine **300** wanaotarajiwa kupewa mafunzo katika awamu ya pili.

**Taasisi zilizo chini ya Sekta ya Uvuvi**

**Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO)**

52. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuvutia uwekezaji wa Serikali na sekta binafsi, TAFICO imeandaa Mpango wa Biashara (*Business Plan*) ambao umeainisha miradi ya kimkakati kwa ajili ya kuongeza tija katika uvuvi wa bahari kuu na mnyororo wa thamani wa mazao ya uvuvi. Pia, katika mpango huo TAFICO itashirikisha sekta Binafsi katika kuibua na kutekeleza baadhi ya miradi kwa utaratibu wa ushirikiano kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (*Public - Private Partnership*).

**Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu**

53. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu imetoa leseni za uvuvi wa bahari kuu kwa meli **48** ambapo meli tatu (**3**) ni za ndani na **45** ni za nje ikilinganishwa na leseni **25** zilizotolewa mwaka 2021/2022**.** Kuongezeka kwa leseni hizi kumeongeza makusanyo kutoka shilingi **bilioni 3.3** mwaka 2021/2022 hadi shilingi **bilioni 6.2** mwaka 2022/2023. Ongezeko hilo limechangiwa na juhudi za makusudi za kufungua mipaka na kuweka mazingira rafiki ya uwekezaji zinazofanywa na **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

54. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, kampuni ya *Albacora Group* ya Uhispania imeshusha hapa nchini tani **100** za samaki wasiolengwa (*by-catch*) pamoja na kufundisha mabaharia wa Kitanzania **10** (**5** kutoka Tanzania bara na **5** Tanzania Zanzibar).

**MIRADI YA MAENDELEO YA SEKTA YA UVUVI**

**I. Miradi ya Maendeleo chini ya Programu ya ASDP II**

55. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Wizara imeendelea kutekeleza Mradi wa ujenzi wa Bandari ya Uvuvi Kilwa Masoko, ambapo usanifu wa kina (*Detailed Design*) umefanyika na kazi ya ujenzi imeanza.

**II. Mradi wa Mkopo wa Masharti Nafuu (*Extended Credit Facility– ECF*)**

56. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Serikali ilitenga Shilingi **bilioni 60** kwa ajili ya kuwawezesha wavuvi kwa kuwakopesha boti za uvuvi **158** kwa wanufaika **2,753** na mradi wa vizimba **613** vya kufugia samaki vyenye wanufaika **3,154** na mkopo wa pembejeo za ukulima wa mwani kwa wanufaika **2,030**.

57. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, sehemu ya fedha hizi zilielekezwa katika kuanzisha mashamba darasa **13** ya ufugaji wa samaki katika Halmashauri za Wilaya **13** kama zilivyoainishwa katika ibara ya **202**.

**III. Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi**

58. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea na taratibu za ununuzi wa meli mbili (**2**) za uvuvi wa bahari kuu zenye vifaa vya kisasa kwa ajili ya Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO).

**Dawati la Sekta Binafsi la Wizara**

59. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka wa fedha 2022/23, Serikali kupitia Benki ya Maendeleo ya Kilimo ilitoa mikopo ya Shilingi **bilioni 17.05** kwenye Sekta za Mifugo na Uvuvi. Kati ya fedha hizo Shilingi **bilioni 13.70** zilitolewa kwa wazalishaji katika sekta ya mifugo na Shilingi **bilioni 3.35** zilitolewa kwenye sekta ya uvuvi.

60. ***Mheshimiwa Spika,*** Mikopo iliyotolewa ilielekezwa kwenye maeneo yafuatayo:-
    (i) Ufugaji wa kuku;
    (ii) Unenepeshaji wa ng'ombe (*fattening*) kwenye miradi **13** iliyopo katika mikoa ya Tabora, Pwani na Manyara;
    (iii) Ununuzi wa mitamba **243** na ujenzi wa mabanda ya kisasa ya ng'ombe;
    (iv) Ufugaji wa Nguruwe: miradi **7** iliyopo katika mikoa ya Pwani na Mara;
    (v) Uzalishaji wa chanjo za mifugo;
    (vi) Ufugaji wa samaki katika mabwawa: mradi **1** uliopo mkoani Pwani;
    (vii) Ununuzi na uuzaji wa samaki kutoka ziwa Victoria zilitolewa kwenye miradi miwili iliyopo Ukerewe; na
    (viii) Ufugaji wa samaki kwenye vizimba, miradi **2** ya uvuvi katika mkoa wa Mara.

61. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania inatekeleza mradi wa *Blue Economy for Growth* (*BE4G25*) wenye lengo la kuinua uzalishaji wa mazao ya mwani na uvuvi wa samaki kwa kutoa mikopo ya gharama nafuu kwa ajili ya ununuzi wa boti za kisasa, ujenzi wa vizimba vya kufugia samaki (*cages*) na utoaji wa ushauri wa kitaalamu. Hadi sasa, maombi **400** kutoka vyama vya msingi (AMCOS), makampuni na watu binafsi tayari yamepokelewa na yanafanyiwa uchambuzi. Mradi huu unatekelezwa katika mikoa yote iliyozungukwa na maziwa makuu (Victoria, Tanganyika, Rukwa na Nyasa) na mikoa inayopakana na Bahari ya Hindi.

**MPANGO WA MWAKA WA FEDHA 2023/2024**

**MAENEO YA VIPAUMBELE KATIKA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2023/2024**

62. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Sekta ya Uvuvi imepanga kutekeleza vipaumbele vinavyoendana na kufungamanisha Uchumi wa Buluu hususan matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi ikiwemo uvuvi wa asili na ukuzaji viumbe maji. Vipaumbele hivyo ni pamoja na:-

    (i) Kuimarisha uwezo wa uvuvi katika bahari

kuu;
(ii) Kuimarisha taasisi za Uvuvi ili kuongeza ushiriki katika Uchumi wa Buluu;
(iii) Kusudio la kuanzisha Mamlaka ya Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi;
(iv) Kuongeza uwekezaji katika miundombinu ya uvuvi na ukuzaji viumbe maji;
(v) Kuimarisha uthibiti wa ubora wa mazao ya uvuvi na masoko.
(vi) Kuimarisha huduma za Ugani wa Uvuvi na Ukuzaji Viumbe maji.

63. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza vipaumbele hivyo, baadhi ya kazi zitakazofanyika katika mwaka 2023/2024 ni pamoja na:-

(i) Kuendelea na ujenzi wa bandari ya uvuvi Kilwa Masoko - Lindi; Ununuzi wa meli tatu (3) za uvuvi wa Bahari Kuu; Kufanya utafiti wa wingi na mtawanyiko wa samaki katika bahari kuu; na kutoa leseni kwa meli za uvuvi wa Bahari Kuu kupitia DSFA.

(ii) Kuimarisha Taasisi za Uvuvi kwa kujenga miundombinu muhimu; kununua boti zenye vioo chini (glass bottom boat) ili kuongeza utalii kwenye Hifadhi za Bahari na maeneo Tengefu (eco-tourism); Kufanya tafiti za kujua wingi, aina na mtawanyiko wa samaki katika Maziwa na Bahari ya Hindi; kujenga vyumba vya mihadhara na vifaa vya kufundishia katika Kampasi tano (5) za FETA.

Aidha, kwa kushirikiana na sekta binafsi TAFICO itajenga viwanda vya kutengeneza chakula cha samaki na kuchakata mazao ya uvuvi, itakarabati gati la kuegeshea meli (*Floating Jetty*); na kununua magari ya ubaridi, kutoa mafunzo kwa Mabaharia kuhusu uvuvi wa Bahari Kuu na kujenga ghala la ubaridi, jengo la mtambo wa kuzalisha barafu na jengo la uhandisi wa mitambo ya uvuvi.

(iii) Serikali inakusudia kuanzisha Mamlaka ya Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi mahususi kwa ajili ya kusimamia na kuendeleza rasilimali za uvuvi kwa lengo la kuongeza ufanisi katika usimamizi, ulinzi na uendelezaji wa rasilimali za uvuvi. Mamlaka hii itawezesha kupunguza au kuondoa changamoto zinazoikabili Sekta ya Uvuvi ikiwa ni pamoja na kukabiliana na uvuvi haramu; Hivyo kuongeza wingi wa samaki, usalama wa chakula, ongezeko la ajira, kipato cha mtu mmoja mmoja na Pato la Taifa. Suala hili ni utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uvuvi ya mwaka 2015 na maelekezo ya Ilani ya CCM Ibara ya 43 (f).

(iv) Kuendelea na ulinzi shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi, Kuimarisha Vikundi vya Usimamizi shirikishi wa Rasilimali za uvuvi, kutoa elimu kwa wavuvi; na kuimairisha vituo vya Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi.

(v) Kuwawezesha wavuvi na wafugaji samaki kupata pembejeo na zana za kisasa za uvuvi ikiwemo boti **160** na vizimba **893** kupitia programu ya mkopo nafuu (ECF); Kujenga mialo, masoko na vituo vya Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi; Kufanya Upembuzi Yakinifu na kujenga soko la samaki Kigamboni, mashamba darasa ya ufugaji samaki; Kuanzisha vituo atamizi **14** kwa ajili ya kuwawezesha vijana **750** kushiriki katika programu maalum ya Atamizi kwa miezi mitatu (**3**). Baada ya mafunzo, vijana hao watawezeshwa kupata pembejeo za ufugaji samaki na kilimo cha mwani kupitia Programu ya ECF; na kuainisha maeneo ya ufugaji samaki kwa vizimba katika maeneo yanayozunguka Ziwa Nyasa, Rukwa na Tanganyika.

(vi) Kuimarisha Maabara ya Taifa ya Uvuvi kwa kuiwezesha vifaa vya maabara na kufanya uchunguzi wa sampuli; Kufanya kaguzi za kuhakiki ubora wa mazao ya uvuvi na kujenga vichanja vya kukaushia dagaa ili kupunguza upotevu wa dagaa baada ya kuvuliwa;

(vii) Kuimarisha vituo vya ufugaji wa samaki kwa kukarabati na kuongeza miundombinu ili kuzalisha vifaranga zaidi vya samaki, Kupandikiza vifaranga vya samaki katika mabwawa ya asili; na Kutoa mafunzo kwa wakulima wa mwani.

64. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuchagiza utekelezaji wa Uchumi wa Buluu, Wizara yangu itashirikiana na Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi ya SMZ pamoja na Taasisi mbalimbali zikiwemo IUCN, Irish Aid, FAO, JICA, UNDP, WB, EU, IFAD, WWF pamoja na Balozi za nchi mbalimbali katika kutekeleza miradi ya Maendeleo.

**Makadirio ya Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka 2023/2024**

65. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Wizara kwa upande wa Sekta ya Uvuvi (**Fungu 64**) inatarajia kukusanya jumla ya Shilingi **bilioni 41.0** kutoka kwenye vyanzo mbalimbali.

**E: HITIMISHO**

66. ***Mheshimiwa Spika,*** kabla ya kuhitimisha hotuba yangu, naomba kuchukua fursa hii kuwashukuru wale wote waliochangia kwa namna moja au nyingine katika kuiwezesha Wizara kufanikisha majukumu yake. Mafanikio yaliyopatikana katika mwaka 2022/2023 yametokana na uongozi bora na mahiri wa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania bila kusahau hamasa na ushiriki wa wananchi wakiongozwa na Waheshimiwa Wabunge na Madiwani.

67. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutumia fursa hii kuwatambua na kuwashukuru Washirika wa Maendeleo waliochangia mafanikio ya Sekta za Mifugo na Uvuvi.

68. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa wananchi wa Jimbo la Mkuranga ambao muda wote wameendelea kuniunga mkono katika kutekeleza majukumu yangu ya jimbo na ya Taifa letu, nataka niwahakikishie kuwa nitaendelea kuwatumikia kwa juhudi na maarifa ili kuleta mabadiliko ya kimaendeleo katika jimbo letu na Taifa kwa ujumla.

**F. MUHTASARI WA MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024**

69. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Wizara inaomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi ya jumla ya Shilingi **295,920,933,000**. Kati ya fedha hizo, Shilingi **112,046,777,000** ni kwa ajili ya Sekta ya Mifugo (Fungu 99) na Shilingi **183,874,156,000** kwa ajili ya Sekta ya Uvuvi (Fungu 64). Mchanganuo wa fedha zinazoombwa kwa kila Fungu ni kama ifuatavyo: -

**Fungu 99: Sekta ya Mifugo**

70. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaomba kutumia jumla ya Shilingi **112,046,777,000** kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Sekta ya Mifugo. Kati ya fedha hizo, Shilingi **50,122,670,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **61,924,107,000** ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Mgawanyo wake ni kama ifuatavyo:-

**(i) Fedha za Matumizi ya Kawaida: Shilingi 50,122,670,000**
- Mishahara Shilingi **23,939,807,000**
- Matumizi Mengineyo (OC) Shilingi **26,182,863,000**

(ii) **Fedha za Matumizi ya Maendeleo: Shilingi 61,924,107,000**
- Fedha za Ndani, Shilingi **56,592,173,000**
- Fedha za Nje, Shilingi **5,331,934,000**

**Fungu 64: Sekta ya Uvuvi**

71. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Wizara inaomba jumla ya Shilingi **183,874,156,000** kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Sekta ya Uvuvi. Kati ya fedha hizo, Shilingi **49,462,296,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **134,411,860,000** ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Mchanganuo wake ni kama ifuatavyo:-

**(i) Fedha za Matumizi ya Kawaida: Shilingi 49,462,296,000.**
- Mishahara ni Shilingi **15,368,951,000**
- Matumizi Mengineyo **(OC)** ni Shilingi **34,093,345,000.**

**(ii) Fedha za Matumizi ya Maendeleo: Shilingi 134,411,860,000**
- Fedha za Ndani: Shilingi **110,682,025,000**
- Fedha za Nje: Shilingi **23,729,835,000**

72. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza.

73. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.

## Sekondari zapewa vifaa vya TEHAMA

**Na Frank Monyo**

MKUU wa Mkoa wa Iringa, Halima Dendego, amepokea msaada wa vifaa 49 vya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) vyenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 89 kwa ajili ya shule 14 kutoka Vodacom Tanzania Foundation.

Msaada huo ni mpango wa uunganishwaji wa shule kwa kushirikiana na Shirika la African Child Projects na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) ambao unalenga kuzifikia shule 300 za umma nchini katika awamu ya pili.

Akizungumza wakati wa hafla fupi ya makabidhiano iliyofanyika katika Shule ya Sekondari Mtwivila juzi, Halima alipongeza mkakati huo wa Vodacom Tanzania Foundation na washirika wake.

Halima aliutaja msaada huo unaakisi malengo ya serikali katika kuboresha sekta ya elimu na mafunzo ya kidijitali nchini.

"Bado kuna uhitaji mkubwa wa wataalamu kwenye sekta ya TEHAMA nchini ambao lazima waandaliwe katika hatua za awali. Mara nyingi wanafunzi huchukia masomo ya michepuo ya sayansi na teknolojia kutokana na kukosa maandalizi mapema na vifaa vya kujifunzia.

"Lakini kwa kuanza kujifunza na kujisomea kupitia vifaa vya TEHAMA wakiwa sekondari, itawajengea uwezo na ari ya kuona kuwa kila kitu kinawezekana," alisema Halima.

Alisema mpango wa kuziunganisha shule na mfumo wa TEHAMA unaleta chachu katika uboreshaji ufundishaji na kujifunza kwa walimu na wanafunzi. Kupitia TEHAMA ni rahisi walimu kuandaa masomo na kuwafikia wanafunzi wengi kwa wakati mmoja.

"Ni matumaini yangu vifaa hivi vya TEHAMA tulivyovipokea kwa hisani ya Vodacom Tanzania Foundation, vitaboresha ufundishaji na kujisomea katika shule zetu. Walimu bila shaka sasa mtakuwa na uwezo wa kufundisha kwa urahisi na kufuatilia kwa ukaribu maendeleo ya wanafunzi wenu.

"Wanafunzi ninawapa changamoto ya kuondoa hofu katika kujifunza, msiviogope vifaa hivi, onyesheni shauku ya kuvifahamu vinatumikaje kwani vitawaandaa kwa masomo yenu kadri mnavyosonga mbele," alisema.

Kompyuta 31, vishikwambi 15, runinga moja na mashine moja ya kutolea nakala vilikabidhiwa kwa shule 14 za sekondari mkoani Iringa.

Shule hizo ni: Tagamenda, Ipogolo, Miyomboni, Iringa Girls, Lugalo, Mkwawa, Mawelewele, Kihesa, Mazoezi, Mlandege, Kwa Kilosa, Mivinjeni Idunda, Mlake na Mtwivila. Mpaka sasa wanafunzi takribani 600,000 wananufaika na mpango huo wa uunganishwaji wa shule nchini.

Mkuu wa Kanda ya Kusini wa Vodacom Tanzania, Happiness Shuma, alisema mradi wa uunganishaji shule nchini ni sehemu ya mkakati wa kampuni yao kutumia mtandao na rasilimali zake kusaidia maendeleo ya jamii.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Mtwivila, Dainess Myala, kwa niaba ya wakuu wa shule zilizonufaika na msaada huo, alishukuru serikali na Vodacom Tanzania Foundation kwa msaada huo.

Programu ya e-Fahamu ilianzishwa na Vodacom Tanzania Foundation mnamo mwaka 2017 kwa lengo la kuwasaidia walimu na wanafunzi wa shule za sekondari kupata vitabu vya ziada na kiada, maudhui ya elimu pamoja na mitaala iliyopitishwa na Taasisi ya Elimu Tanzania na masomo ya kimataifa bure kwa njia ya mtandao. Lengo la tovuti hiyo ni kuunga mkono Mpango wa Serikali wa Kutoa Elimumsingi Bila Ada, maarufu Elimu Bure. Ulianza kutekelezwa rasmi mwaka 2016.

# RC aagiza uchunguzi mishahara isiyozingatia viwango elekezi

**Na Mary Mosha,** MOSHI

MKUU wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, ameagiza kufanyika uchunguzi wa kina kuhusu mashirika binafsi yanayodaiwa kupuuza ulipaji wa mishahara kwa viwango vilivyoelekezwa na serikali.

Wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani juzi mjini Moshi, Babu alimwagiza Katibu Tawala wa Mkoa, Tixon Nzunda, kuchunguza ili kuyabaini mashirika hayo na kuchukua hatua kutokana na unyonyaji wa jasho la wafanyakazi.

"Ninamwagiza RAS (Katibu Tawala wa Mkoa) kufuatilia mashirika binafsi yanayopuuza viwango na kima cha chini cha mshahara vilivyowekwa na serikali ili kuepusha kuwanyonya wafanyakazi.

"Pamoja na hilo, pia ninamwagiza kuifuatilia Idara ya Kazi Mkoa kutokana na malalamiko ya wafanyakazi kwenye risala yao kwamba idara hiyo imeshindwa kusikiliza matatizo ya wafanyakazi na kuyatatua kwa wakati," alielekeza.

Babu alisema kushindwa kutekeleza maagizo ya serikali ni uvunjifu wa sheria, hivyo ni lazima hatua stahiki zichukuliwe.

Kwa mujibu wa Babu, kutolipa viwango vya mishahara vilivyopangwa na serikali ni ukiukwaji wa Sheria ya Ajira ya Mwaka 2004.

Awali, Mratibu wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi (TUCTA) Mkoa wa Kilimanjaro, Kanuti Magashi, alisema wafanyakazi wanakabiliwa na vikwazo vingi na wanapowasilisha kero zao Idara ya Kazi, hawapati haki katika idara hiyo.

"Katika kufikia ufanyaji wa kazi kwa morali, tunaomba serikali iangalie maisha yalivyopanda, utatuaji wa matatizo ya wafanyakazi kwa wakati na wenye staha na vima vya chini kuangaliwa hasa kwenye mashirika binafsi," alisema mratibu huyo.




Kaimu Mkurugenzi wa Mawasiliano wa Benki ya CRDB, Emmanuel Kiondo, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana kuhusu kufungwa kwa dirisha la maombi ya mitaji kwa wabunifu na wajasiriamali wanawake inayotolewa na benki hiyo chini ya Programu ya IMBEJU. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kanisa latoa vifaa vya matibabu hospitalini

**Na Mary Geofrey**

KANISA la The Word of Reconciliation Ministries (WRM) limeitumia Siku ya Wafanyakazi Duniani 'Mei Mosi' kuchangia damu, kupandaji miti na kutoa vifaa vya matibabu kwa wagonjwa katika Hospitali ya Wilaya iliyoko Kivule mkoani Dar es Salaam.

Katika kuungana na serikali inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan, kanisa hilo chini ya kiongozi wake, Nabii Nicholaus Suguye aliyefuatana na viongozi na waumini wa kanisa hilo na washiriki kuchangia damu, kufanya usafi na kukabidhi vifaa hivyo.

Nabii Suguye alisema wameamua kufanya hivyo ikiwa ni sehemu ya ushiriki wao kwa jamii ya Kivule na kurudisha matumaini kwa wagonjwa, pia kuiunga mkono serikali katika kuisaidia jamii.

Aliipongeza serikali kwa majengo ya kisasa yaliyoko katika Hospitali ya Wilaya ya Ilala na kutoa wito kwa wadau mbalimbali kushirikiana na serikali katika kuisaidia jamii.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Wilaya ya Ilala, Dk. Nyamboto Thobias alishukuru kwa msaada huo na kuelezea namna walivyofarijika.

Aliahidi vifaa hivyo vitakwenda kuwasaidia wagonjwa wa hospitali hiyo huku baadhi ya washiriki katika shughuli ya usafi, upandaji miti na kuchangia damu wakisisitiza umuhimu wa kutunza mazingira.

Dk. Thobias alibainisha kuwa kanisa hilo limewapa vifaa mbalimbali vya matibabu ikiwa ni pamoja na giving set infusion pc 500, sababu na sindano.

Alisema hospitali hiyo kwa sasa ina majengo 13 yaliyokamilika ikihudumia wastani wa wagonjwa 200 kwa siku. Wanaendelea na ujenzi wa majengo mengine.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**Probate and Administration Cause No.41 of 2023**
**In the matter of the Estate of the late ANOLD PHILIMON KILONGANYA of Mnadani Ward within Dodoma City**
**And**
**In the matter of application for letter of administration by ANNA ANOLD KILONGANYA**
**PETITION FOR LETTER OF ADMINISTRATION WHEN THE DECEASED DIED INTESTATE (SECTION 56).**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules GN. NO.369 of 1963)**

**All PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 7 Day of 6, 2023

Dated at Dodoma this 2 day of MAY, 2023

RESIDENT MAGISTRATE

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**BENJAMIN DANIEL FISSO** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya TOYOTA LANDCRUISER yenye jina la umiliki MAMA SAVANA SAFARIS COMPANY LTD yenye usajili namba T341 AEJ , CHASSIS NAMBA: HZJ750005182 na EGNINE NAMBA: 1HZ0029237 . kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:
**ARU/ARU/RB/150901/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**BENJAMIN DANIEL FISSO** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya TOYOTA LANDCRUISER yenye jina la umiliki ANTELOP SAFARIS LTD yenye usajili namba T574 ABP , CHASSIS NAMBA: HZJ750038696 na EGNINE NAMBA: 0319144 . kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:
**ARU/ARU/RB/150922/2023**

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 44 OF 2023**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE ANJELIKA ADOLF NDONJEKWA**
**AND**
**IN THE MATTER OF APPLICATIONFOR LETTERS OF ADMINISTRATION**
**BY: - 1. FELICIAN MASOLWA KAPAMA**
**2.THOMAS FRANCIS**
**GENERAL CITATION**
**(RULE 75 OF PROBATE RULES GN.369 OF 1963)**

ALL PERSONS Claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Admiration is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 18th Day of MAY, 2023.

Dated at Dodoma this 19th day of APRIL, 2023

PETITIONER

PRINCIPAL/SENIOR /RESIDENT MAGISTRATE

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**FLORAH RAPHAEL MDIMA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA HILUX** yenye usajili namba: **T 144 AEA,** CHASSIS NAMBA: **LN1060064664.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:
**SOG/RB/2255/2023**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

Ndugu **JOSEPH MUJWAHUZI MUSHUMBUSI** anatangaza kupotelewa na kadi yake ya gari aina ya (Excavator) yenye namba za usajili **T 779 DCG.** Ametoa taarifa polisi na kupewa namba **MOR/MOR/RB/143328/2023** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**GS GROUP LIMITED** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki aina ya **HAJUE H125-8EX** yenye usajili namba: **MC 469 CNS,** CHASSIS NAMBA: **LC6PCJK23L0011925.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:
**SOG/RB/3359/2023**

**FOMU MIRATHI - 2**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya TEMEKE**
**Kituo cha JUMUISHI Mkoa DAR ES SALAAM**
**Usimamizi wa mirathi Na. 642/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU MWINYI ABDALLAH WA JIHAD**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA JEHAD ABDALLAH JEHAD**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 29 Mwezi 05 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

Imetolewa leo tarehe 02 Mwezi 05 Mwaka 2023.

HAKIMU

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JIMBO LA MBINGA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA LANDCRUISER** yenye usajili namba: **T 802 AAC,** CHASSIS NAMBA: **JTELB715907027868.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:
**SOG/RB/3360/2023**

## KUPOTEA KWA CHETI



**JOFREY WILFRED MSWANJELE** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA CHETI CHA KIDATO CHA NNE CHENYE INDEX NAMBA S.5304/0034 KILICHOTOLEWA NA BARAZA LA MITIHANI LA TAIFA KUPITIA MPESU SEKONDARI MWAKA 2019.YEYOTE ATAKAYEKIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.TAARIFA YA POLISI **MBE/MBE/RB/128931/2023**

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**RAMADHANI SHAIBU CHIGOGOLO, MKAZI WA DAR ES SALAAM, AMEPOTEZA HATI YA KUSAFIRIA YENYE NAMBA TAE123421** iliyotolewa tarehe 19/06/2019 na mamlaka ya uhamiaji tanzania. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: DAR/CHA/RB/150332/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ROSEMARY JOHN HAULE** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **MITSUBISH CANTER** yenye usajili namba: **T442 AVQ,** CHASSIS NAMBA: **FEB637EA00072.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:
**SO/RB/1031/2023**


## OFISI ZA MATANGAZO

MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.
MOB: +255 - 0677020701
E-mail: advertise@guardian.co.tz,
Website: www.ippmedia.com

## Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

SIKU YA UHURU VYOMBO VYA HABARI

# Wenye fani Zanzibar walilia marekebisho kisheria, wasimamizi wajibu; iko njiani

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR



Waandishi habari wa Zanzibar, wakiwa kazini kufuatilia mada inayowahusu. **PICHA: MTANDAO**

WAKATI dunia inaadhimisha Siku ya Uhuru wa Habari, bado uhuru wa kujieleza na kupata habari visiwani Zanzibar inadaiwa kupitia misukuko, hali inayosababisha wananchi wakiwamo vijana kukosa taarifa muhimu, ambazo kama wangezifikia zingesaidia katika kufanya maamuzi sahihi.

Licha ya kifungu cha 18 cha Katiba ya Zanzibar ya 1984 kutoa uhuru wa kujieleza na kutoa maoni, kuna sheria mbili zinazosimamia sekta ya habari; Sheria ya Tume ya Utangazaji ya 1997 na Sheria ya Wakala wa Usajili wa Habari, Magazeti na Vitabu ya 1988, zinalalamikiwa.

Haiko katika kukandamizwa uhuru wa kujieleza na kutoa maoni sio tu kwa waandishi wa habari, bali hata makundi mengine, wakiwamo vijana, ukitolewa mfano Kifungu cha 27 Sheria ya Wakala wa Usajili wa Habari, kinampa mamlaka ofisa yeyote wa polisi, kuvamia nyumba kama atadhani kuna gazeti linachapishwa.

Jabir Idrissa, mwandishi wa habari mwandamizi, anasema kifungu hicho kinaeleza uwezo wa kukamata magazeti na kupekua majengo, huku akitaja pia kifungu cha sheria kinachopangilia uhuru wa habari, pale ofisa wa polisi anaweza kukamata gazeti lolote lililochapwa au kuchapishwa, ambalo kwa maoni yake atalituhumu kuwa kinyume na sheria hiyo.

Pia anataja sheria inampa nguvu hakimu kutoa hati kumruhusu ofisa wa polisi wa cheo cha mkaguzi au cha juu, akiwa na msaada au bila ya msaada, au kuingia na kupekua sehemu yoyote, ambayo kwa maoni yake anadhani limo gazeti lililochapwa kinyume na sheria hiyo.

Jabir anayataja kuwa ni mapungufu yanayohitaji kufanyiwa marekebisho, wanahabari kufanya kazi zao kwa weledi bila ya kuingiliwa.

Shifaa Said, ni Ofisa Mwandamizi kutoka Baraza la Habari Tanzania (MCT), anasema kuna baadhi ya vifungu katika sheria hiyo, sio rafiki kwa waandishi wa habari, hata kuwafanya waandishi kufanya kazi kwa woga.

"Hivi sasa wadau wa habari tumeshajadili mapungufu yaliyomo ndani ya sheria hiyo na kutoa maoni yetu ili mwisho wa siku maoni hayo yawasilishwe na kuwa na sheria rafiki kwa waandishi wa habari," anasema.

Zaina Abdallah Mzee, ni mratibu wa mradi wa kuboresha habari unaoendeshwa na Shirika la Internews Tanzania kwa kushirikiana na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA), anasema wameamua kuungana kupaza sauti, ili sheria bora zisizokandamiza uhuru wao kujieleza zifikiwe.

Pia anawataka waandishi wa habari na wadau visiwani Zanzibar, kuziibua sheria zingine kandamizi kwa habari kwao, wapeleka maoni yao katika sehemu husika na kufanyiwa marekebisho.

"Suala la kupata, kusambaaza habari lipo kikatiba zaidi sasa kama sheria imetungwa inakinzana na haki hiyo, haina nafasi kwa sasa inahitaji kufanyiwa marekebisho,"anasema.

Zuhura Juma, mwandishi wa habari wa Shirika la Magazeti Zanzibar, akiwa Pemba, anasisitiza kifungu hicho tajwa kinapaswa kufanyiwa marekebisho haraka, kwa sababu kinampa mamlaka makubwa polisi dhidi ya chombo cha habari, hata inawafanya waandishi, vijana, wauza magazeti, wasambazaji na kampuni zake kuishi katika hofu.

"Kama kuna mamlaka inahisi gazeti au chombo chochote cha habari kimeandika vibaya au limekwenda kinyume na sheria za habari, vizuri kufuata taratibu za kisheria na sio kuwakamata moja kwa moja au kuwavamia," anasema.

Juma Khamis, Mwanasheria wa shirika hilo la magazeti, anasema kuna sheria nyingi zinazominya uhuru wa habari na wa kujieleza, ikiwamo Kifungu cha 127 cha Sheria ya Uchaguzi Zanzibar.

"Ni vyema kipengele hiki cha sheria ya uchaguzi kikafanyiwa marekebisho ni kieleze wazi ni watu wa aina gani wasiopaswa kufanya, hivyo kuliko kusema ni mtu yeyote ambapo waandishi wa habari pia wamejumuishwa," anasema mwanasheria huyo, akitoa mfano linganifu wa nchi za Afrika kama Nigeria, Kenya na mashirika nchini Afrika Kusini, yanafanya hesabu zao kutangaza matokeo bila ya kizuizi chochote kiasheria.

Shadida Said, Mwanasheria kutoka Mtandao wa Mtetezi wa Haki za Binadamu Tanzania Ofisi ya Zanzibar, anasema sheria kumpa nguvu ofisa wa polisi kukamata na kupekua, ni kipimo kikubwa cha ukiukwaji uhuru wa habari nchini na kujieleza.

> "Sisi viziwi bila ya lugha ya alama hatuwezi kupata mawasiliano na vyombo vingi vya habari havina wakalimani lakini hata tunapotaka kupata taarifa katika taasisi mbalimbali nako hali ni hiyo hiyo.

## WASHIRIKA WA WANAHABARI

Abdallah Alawi, mwenye ulemavu wa uziwi, anasema uhuru wa kujieleza kupata habari unasaidia kukuza demokrasia nchini, lakini bahati mbaya umeminywa, akilalamika wanakosa haki ya kupata taarifa kwa kutokuwapo wakalimani wa lugha ya alama.

"Sisi viziwi bila ya lugha ya alama hatuwezi kupata mawasiliano na vyombo vingi vya habari havina wakalimani lakini hata tunapotaka kupata taarifa katika taasisi mbalimbali nako hali ni hiyo hiyo," anasema Alawi.

Abdalllah Mussa Hija, kutoka Jukwaa la Vijana Zanzibar, anasema uhuru wa kujieleza vijana una vikwazo, licha ya kupata nafasi ya kutuma taarifa zao, ikiwamo katika mitandao ya kijamii na vyombo vya habari, akitaja vinavyojumuisha vijana kukoseshwa taarifa sahihi, wanapoenda kuhoji kuanzia ngazi za Shehia (kata), kuhusu suala la maendeleo, kwenye halmashauri au ofisi za wilaya viongozi wa taasisi huwa wagumu kutoa taarifa.

Anasema ni inayochangiwa na Zanzibar kutokuwa na sheria ya moja kwa moja kumlazimisha mtoa taarifa kueleza hitaji la habari kwa umma. Hapa anaendelea: "Wakati mwingine vijana wanapotumia mitandao ya kijamii kuna baadhi ya taarifa huwa kikwazo kwa serikali na vijana kuingia katika utata kwenye vyombo vya sheria ikiwamo Jeshi la Polisi."

Anafafanua, hata waandishi wa habari wanapoenda kutafuta taarifa katika baadhi ya idara, hawapatiwi kwa usahihi, akiwa na rai kwamba marekebisho ya Sheria ya Wakala wa Usajili wa Habari, Magazeti na Vitabu ya 1988 yakifanyika, yatafungua mwanya katika haki ya kupata taarifa.

Naye anakumbusha dai la wanahabari kila mtu kupatiwa taarifa sahihi pale anaphotaji, pasipo vizingiti, ili wigo wa uhuru kujieleza na haki ya kupata taarifa ikae vyema.

Ali Sultani Seif, Ofisa Vijana Wilaya ya Kati Unguja, anasema bado uhuru wa kujieleza ni changamoto, kwa sababu wadau wa maendeleo yao hawapatiwi taarifa na za kuziridhisha, huku wakishindwa kuvitumia vyombo vya habari kutoa maoni yao, ili kuifika serikalini na jamii.

Rai yake ni vijana wajumuishwe katika masuala yanayowahusu, kwa sababu taifa linawategemea wao, nguvu kazi wa ajili ya maendeleo.

## 'WAZITO' SMZ WAFAFANUA

Katibu Mtendaji Tume ya Kurekebisha Sheria wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Mussa Kombo, anasema mchakato wa marekebisho ya sheria ya habari haukupitia tume yao, lakini sheria hiyo inamuda mrefu, inahitaji kufanyiwa marekebisho.

"Sisi kama Tume ya Kurekebisha Sheria, moja ya majukumu yetu ni kurekebisha sheria ambazo wadau wanaona zimepitwa na wakati, lakini kwa sheria hii ya habari haijapitia kwetu na imeenda moja kwa moja katika ngazi za juu," anasema.

Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo Zanzibar, Tabia Maulid Mwinyi, anasema mchakato wa kuifanyia marekebisho sheria hiyo ya habari, imefikia hatua bora kwa sasa ipo katika ngazi ya makatibu wakuu.

Anasema, tayari wameshapokea maoni ya wadau wa habari kuhusu marekebisho ya sheria na serikali itayafanyia kazi maoni hayo, ili kuwa na sheria isiyo na kikwazo kwa uhuru wa habari, pia wa kujieleza.

"Baada ya marekebisho ya sheria hii kutoka kwa makatibu wakuu, itakwenda kwa Mwanasheria Mkuu, Baraza la Mawaziri na kisha litasomwa katika kikao cha Baraza la Wawakilishi na wala haitachukua muda mrefu, itawasilishwa barazani,"anaahidi waziri.

# Wenye fani watabasamu wakihesabu orodha uungwana wa Rais Samia kwao

## ●Ruksa kukosoa serikali, waliofungiwa huru, sheria mpya, gharama nafuu mtandaoni...



Viongozi wa Jukwaa la Wahariri, wakimsikiliza Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari (picha ndogo), Nape Nnauye, wakati wa Mkutano wa 12 wa Mwaka wa Kitaaluma wa Wahariri, katika hoteli ya Morena mkoani Morogoro, Machi 29 mwaka huu. **PICHA: MTANDAO**

**Na Jenifer Gilla**

MAADHIMISHO ya Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari Duniani, hufanyika kila siku ya Mei 3 ya mwaka, ambao mwaka huu kitaifa yatatimiza miaka 30 na yatafanyika Zanzibar, huku mgeni rasmi akitarajiwa kuwa Rais Dk. Hussein Mwinyi.

Mkurugenzi wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake nchini (TAMWA), Rose Ruben, anasema lengo lake ni kukuza uelewa wa umuhimu wa vyombo vya habari nchini kuheshimu namna inavyolindwa katika Ibara ya 19 ya tamko la Haki za Binadamu duniani.

Anasema mwaka huu maadhimisho yamejikita katika kuhimiza uwapo wa uhuru wa vyombo vya habari na uhuru wa kujieleza, kama haki muhimu kwa binadamu na nyenzo muhimu ya kukuza na kuimarisha sekta ya habari nchini.

Mjumbe wa Kamati ya Utendaji ya Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Neville Meena, anautaka uhuru wa vyombo vya habari, umekuwa nchini katika kipindi cha miaka miwili ya uongozi wa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, vyombo vinatekeleza majukumu yake kwa weledi, bila kuwa na hofu ya kufungiwa au kuwekwa maisha yao rehani watakapoandika jambo linaloihusu serikali.

"Tukienda kwenye uhalisia bado hatujasikia chombo cha habari kufungiwa, kasi ya kufungia vyombo vya habari imepungua na vile vilivyofungiwa, vilifunguliwa kama vile Mawio, Mwanahalisi na Tanzania Daima, ni mafanikio makubwa kwenye tasnia ya habari," anasema Neville.

Anafafanua kuwa ni mabadiliko anayotaja yamesababishwa na rais mwenyewe, baada ya kuvipa rungu vyombo vya habari kuikosoa serikali pale inapokwenda kinyume, kauli yake baada ya kuingia madarakani.

"Mwenendo wa rais nao umechangia kubadilisha tabia za watendaji wa serikali, kwamba na wao sasa, wanaanza kuviona vyombo vya habari kama sehemu muhimu ya kuuhabarisha umma na sio maadui hii inaonyesha namna gani serikali hii haiamini vita na vyombo vya habari,"anasema.

Meena anasema, ni mabadiliko yanayoleta maendeleo makubwa ya tasnia uandishi kwa kipindi cha muda mfupi, waandishi hawana woga kufanya uchunguzi wa mambo kuuhabarisha umma, ikiwa na mafanikio.

Vilevile anataja hatua ya serikali kukubali kufanya marekebisho, sheria ya vyombo vya habari na muswada wenye mapendekezo ya maboresho ya sheria, yalisomwa bungeni kwa mara ya kwanza Februari 10 mwaka huu, ingawa analalamikia baadhi yake mependekezo yametolewa.

Pia, anafafanua kuwapo baadhi ya watendaji serikalini, wako katika mtazamo hasi kwa vyombo vya habari, kuviona 'kundi la wahalifu' hata wanatumia nafasi zao kuzuia mabadiliko yanayogusa uhuru wao, lakini kwa majumuisho yake hatua iliyofikiwa inaleta matumaini makubwa.

"Kitendo cha Muswada (wa sheria) kusomwa kwa mara ya kwanza, tunaona tunapiga hatua na kuwa Waziri (Nape Nnauye), akasema milango ipo wazi kwa ajili ya ajili ya majadiliano yoyote tutatumia nafasi hii kuhakikisha mapendekezo yote tuliyoawasilisha kwao yanaingizwa kwenye muswada na kufanyia kazi," anasema.

### MAUDHUI YA MAPENDEKEZO

Meena, anasema uhuru wa vyombo vya habari umeongezeka kwa kiasi kikubwa, lakini bado kuna mambo yanahitajika kufanyiwa marekebisho, ili vyombo vya habari vitekeleze majukumu yao kwa weledi, ikiwamo baadhi ya vipengele vilivyotolewa kwenye Muswada wa Sheria ya Habari, vinarudishwa kwa kuwa ni muhimu.

Anaiomba serikali iondoe ukomo wa chini wa adhabu kwa vifungu vyote, kwa kuwa inambana hakimu wakati wa kufanya uamuzi. Meena, pia anapendekeza kuboreshwa kifungu cha Sheria ya Habari kinachoeleza kuwa serikali inaweza kutoa agizo habari mahsusi kuchapisha au kutangazwa, kwa kuwa ina umuhimu kwa Taifa, akidai hilo inaingilia uhuru wa uhariri.

Pia, anataja kuwapo kifungu cha sheria kinachompa mamlaka Mkurugenzi wa Idara ya Habari (Maelezo) kukataa maombi ya leseni au kuhuisha kulingana na matakwa yake, anapoona chombo husika hakina mwenendo, kwamba kinahitaji kifanyiwa marekebisho.

Kwa mujibu wa Meena, kuhakikisha wanapigania vipengele vilivyotolewa katika muswada Aprili 14, mwaka huu, Timu ya Wadau wa Haki ya Kupata Habari (CoRI), ilitua jijini Dodoma kufafanua zaidi mapendekezo ya mabadiliko ya vipengele vya sheria viliyoachwa nje kwenye Muswada wa Habari.

### KUTOKA MISA -TAN

Mwenyekiti wa Taasisi ya Vyombo vya Habari Kusini mwa Afrika (MISA-TAN) Salome Kitomari, anahimiza dhana ya kuhakikisha wabunge wanaelewa zaidi dhamira ya wanahabari na uhuru wa habari nchini, akisema kwa sasa kuna ukaribu wa serikali kufanya kazi na vyombo vya habari, pia wadau wa habari nchini.

Hapo Salome anajumuisha na suala la upatikanaji taarifa, kwamba umeimarika kwa taasisi n awatu binafsi wanajieleza pasipo hofu, kwa sababu kuna uhuru wa kujieleza.

"Misa Tanzania ambao jukumu letu la msingi ni uhuru wa habari na upatikanaji wa taarifa, tumeona mabadiliko makubwa na ya kuridhisha sana, tunaona ustawi wa wananchi kwenye kutoa mawazo yao kwenye mitandao ya kijamii na maeneo mbalimbali bila kutishwa au kukamatwa na wasiojulikana," anasema.

Katika hilo, anarejea idadi ya vyombo vya mtandaoni vimeongezeka kwa waandishi wamejiajiri, kutokana na kupungua gharama za kumiliki chombo cha mtandaoni, vyote ni zao la jitihada za Rais Samia kuona waandishi wanaifurahia nchi yao.

"Ingawa mabadiliko yaliyofanyika kwenye sheria ni madogo, tofauti na matarajio ya wadau wa habari na waandishi, lakini tunaamini ni mwanzo, kadri tunavyozungumza na kuelimishana, kuna wakati maofisa wa serikali wataelewa umuhimu wa mabadiliko kwenye vifungu tunavyoona vinahitaji mabadiliko," anasema.

Salome anataja kuwapo changamoto ya waandishi wa vyombo vya mtandaoni kushindwa kumudu gharama za usajili, hivyo anashauri iapowezekana Rais aone iwezekano wa huduma hiyo kuwa bure, kwa sababu dunia inaoelekea, huduma intaneti itakuwa bure, hata kumwezesha mtu kumiliki chombo cha habari kokote aliko.

Mwenyekiti huyo anataja jingine la madeni ya muda mrefu yatokanayo na huduma za vyombo vya ni muhimu yakalipwa kupunguza ugumu kiuchumi, unaovikabili vyombo hivyo nchini, akisema uwapo wa kamati kuangalia hali ya vyombo vya habari kiuchumi na muhimu kuangalia uwezekano wa kutoa ruzuku wa vyombo vya habari.

### KUTOKA SERIKALINI

Akizungumza na waandishi wa habari kuhusu Kamati ya Kuchunguza Uchumi wa Vyombo Vya habari Aprili 22, mwaka huu, Mkurugenzi wa Idara ya Habari Maelezo na na Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa akatamka ahadi kwamba, serikali itavilinda uhuru wa vyombo vya habari, kwa kuwa lengo ni kuona sekta hiyo inakuwa imara na linatekeleza majukumu yake vile inavyotakiwa.

"Niendelee kuwahakikishia tu kuwa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan, inaendelea kulinda uhuru wa vyombo vya habari, pamoja na kulinda uhuru wa vyombo vya habari tunataka kuhakikisha vinastawi na vinashamiri," anahitimisha.

## ZISIKUPITE

### SAM ATAJWA WEST HAM

KLABU ya Leeds United inafikiria kumteua kocha wa zamani wa West Ham na Everton, Sam Allardyce, ambaye amewahi kuiona England mara moja, ili kumrithi Javi Gracia kama kocha mkuu wa klabu hiyo. ***(Athletic)***

### ARTETA KUTETA NA RICE

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta, anataka kufanya mazungumzo na kiungo wa kati wa West Ham, Declan Rice, 24, mwishoni mwa msimu huu. ***(Mirror)***

### GUEHI AFIKIRIWA ARSENAL

ARSENAL inafikiria kumsajili mlinzi wa Crystal Palace na England, Marc Guehi, 22. ***(Mail)***

### POCHETTINO SAFI CHELSEA

CHELSEA inakaribia kumpa mikoba kocha wa zamani wa Tottenham Hotspur na Paris St-Germain, Mauricio Pochettino, kuwa kocha wa kudumu wa klabu hiyo. ***(90Min)***

### RATCLIFFE NA UNITED

JITIHADA za Sir Jim Ratcliffe za kutaka kuwa na hisa nyingi katika Klabu ya Manchester United ni pamoja na kutaka udhibiti wa haraka wa masuala ya uhamisho iwapo mkataba utafikiwa. ***(Telegraph)***

### VILLA NAO WAMTAKA

ASTON Villa ina uhakika inaweza kumsajili mchezaji wa kimataifa wa England, Tammy Abraham kutoka AS Roma - licha ya klabu kadhaa kubwa za Ulaya kuwinda nyota huyo. ***(90Min)***

### WATKINS NA MKATABA

KLABU ya Aston Villa imeanza mazungumzo na mshambuliaji wa England, Ollie Watkins, 27, kuhusu kuongeza mkataba wa mchezaji huyo. ***(Athletic)***

### WARD-PROWSE ASUBIRIWA

TOTTENHAM Hotspur na Newcastle United ni miongoni mwa klabu zinazosubiri kuona bei ambayo Southampton itaweka kwa ajili ya kiungo wa kati wa England, James Ward-Prowse, 28, iwapo timu hiyo itashuka daraja. ***(Mirror)***

### SILVA RUKSA KUONDOKA CITY

KLABU ya Manchester City haitamnyima kiungo wa kati wa Ureno, Bernardo Silva, mwenye umri wa miaka 28, ruhusa ya kuondoka katika klabu hiyo iwapo ataamua hivyo msimu wa majira ya joto. ***(90Min)***

### ABRAHAM AWINDWA UNITED

MANCHESTER United ilituma wasaka vipaji kumtazama mshambuliaji wa AS Roma, Tammy Abraham, 25, mwishoni mwa wiki iliyopita huku klabu hiyo ikifikiria mbadala wa mshambuliaji wa Tottenham Hotspur na England, Harry Kane, 29. ***(Mirror)***

### OLISE ASHTUA PALACE

KOCHA wa Crystal Palace, Roy Hodgson, anaamini Mwenyekiti wa Eagles hao, Steve Parish, anapaswa kuwa na wasiwasi kuhusu klabu kadhaa kumtaka winga Mfaransa Michael Olise, 21, msimu huu wa majira ya joto. ***(Evening Standard)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# LAMPARD: NATAKA KUBAKI HAPA NIIBADILISHE CHELSEA

**LONDON,** England

FRANK Lampard amesisitiza kuwa bado anapenda kuwa Chelsea na anafurahia changamoto ya kuibadilisha klabu hiyo.

**Lampard amepoteza michezo yake yote mitano tangu aliporejea katika klabu hiyo mapema mwezi uliopita kwa kipindi cha pili kama kocha, wakati huu akiwa kama mlezi, baada ya Graham Potter kutimuliwa.**

Chelsea walizomewa kipindi cha mapumziko wakati wa kipigo cha mabao 2-0 nyumbani kwa Brentford wiki iliyopita, ambacho kiliendeleza msururu wao wa kutoshinda katika michuano yote hadi mechi nane, na kukaa nyuma kwa pointi sita kutoka kwenye 10 bora ya Ligi Kuu England.

Jana Jumanne walikuwa wanacheza na Arsenal wanaowinda taji na alipoulizwa kama bado anafurahia kufanya kazi, Lampard alisema: "Hakika. Macho yangu yalikuwa wazi nilipoingia kwenye kazi hii.

**●●● Ninafurahia changamoto hii na nilifahamu sana inakuja, najivunia kuisimamia, napenda kuwa...**

"Nina uzoefu mkubwa katika soka kama mchezaji na sasa kama kocha kuelewa kwamba mambo si lazima yabadilike usiku kucha katika suala la matokeo na tumeliona hilo.

"Kazi yetu ni kufanya kazi juu ya maonesho na mawazo ya kikundi katika mafunzo ili kujaribu kurudisha hisia nzuri. Hiyo inakuja tu na bidii.

"Ninafurahia changamoto hii na nilifahamu sana inakuja. Ninajivunia kusimamia klabu. Ninapenda kuwa hapa na ninafurahia kufanya kazi yangu.

"Ukweli katika soka ni kwamba kazi yako haitakuwa na mafanikio kila mara. Watu daima watakumbuka mafanikio, lakini sehemu ya kazi ni nyakati ngumu zaidi, iwe meneja au mchezaji.

"Huwezi kudhibiti matokeo kila wakati, lakini unaweza kudhibiti jinsi unavyofanya kazi kila siku, kwa hiyo ninafurahia kipengele hicho."

Matumaini ya Chelsea katika Ligi ya Mabingwa Ulaya pia yamezimwa chini ya Lampard baada ya kushindwa kwa jumla ya mabao 4-0 na Real Madrid.

"Hatuko katika wakati mzuri, sivyo?" Lampard alisema. "Lakini nimeweza kuishi hivi sasa kwa wiki chache. Pia niliishi labda miaka 10 ya mafanikio ya ajabu hapa na nikaona ikiendelea na nilikuwa sehemu yake tena na nikaona ikiendelea.

"Inaweza kuwa ya kawaida sana, ukiangalia historia ya klabu zote kubwa kwenye ligi, kuna nyakati nzuri na ngumu."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,109,9

JACKPOT
MECHI WIKI HII
TAREHE: 3 NA 4 MEI 2023
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 03/05/23 | 20:00 | Mjallby vs AIK Football | 2.77 | 2.93 | 2.45 |
| 02. 03/05/23 | 20:00 | Sparta Prague vs Slavia Prague | 2.31 | 3.22 | 2.80 |
| 03. 03/05/23 | 20:00 | Panathinaikos vs PAOK | 2.29 | 2.98 | 3.30 |
| 04. 03/05/23 | 20:30 | Valencia vs Villarreal | 2.90 | 3.30 | 2.26 |
| 05. 03/05/23 | 21:45 | Stuttgart vs Eintracht Frankfurt | 2.42 | 3.39 | 2.85 |
| 06. 03/05/23 | 21:45 | Burton vs Cambridge Utd | 2.97 | 3.22 | 2.31 |
| 07. 03/05/23 | 23:00 | Getafe vs Celta Vigo | 2.50 | 2.90 | 2.90 |
| 08. 04/05/23 | 01:00 | CD Palestino vs San Lorenzo | 2.90 | 3.01 | 2.36 |
| 09. 04/05/23 | 03:00 | Colo Colo vs Boca Juniors | 2.37 | 3.08 | 2.83 |
| 10. 04/05/23 | 03:00 | Club Guarani vs SC Emelec | 2.37 | 3.11 | 2.80 |
| 11. 04/05/23 | 20:00 | Norrkoping vs Hammarby | 2.52 | 3.33 | 2.42 |
| 12. 04/05/23 | 21:45 | Empoli vs Bologna | 2.95 | 3.10 | 2.33 |
| 13. 04/05/23 | 21:45 | Huddersfield vs Sheffield Utd | 2.45 | 3.20 | 2.70 |

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money

SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# MAN CITY KILA MECHI NI FAINALI - ALVAREZ



**MANCHESTER,** England

JULIAN Alvarez amekiri "kila mechi ni fainali" baada ya Manchester City kurejea kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu England kwa mara ya kwanza tangu Februari mwaka huu.

Man City mwishoni mwa wiki waliibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Fulham na kupaa kileleni mwa msimamo huo, huku Alvarez akifunga bao la ushindi.

Alvarez ambaye ni mchezaji wa kimataifa wa Argentina, ameiambia tovuti ya City: "Hapa ndipo tulipotaka kuwa mwanzoni mwa msimu.

"Kila mtu amefanya kazi nzuri na sasa tumefika kileleni tunahitaji kuilinda nafasi hii. "Kila mchezo ni fainali kwetu na kila mmoja ataungana kufanya bidii hiyo hadi mwisho."

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, ambaye amelazimika kusubiri nafasi kwenye kikosi cha kwanza cha Pep Guardiola, aliongeza: "Ilikuwa nzuri sana kufunga hapa.

"Bao muhimu sana katika hatua muhimu ya mechi. Ni vizuri kuchangia.

"Tulijua isingekuwa rahisi kuja hapa kwa sababu ya uwanja, kwa sababu ya jinsi Fulham walivyo wazuri kama timu. Tulifurahi sana kuhimili shinikizo na kustahimili."

"Tulikuwa na mpango wazi wa mchezo. Tulitaka kupitia katikati ya uwanja, huku mawinga wetu wakiwa ndani zaidi.

"Ukijaribu kuzuia baadhi ya maeneo watatafuta kuficha wengine, wachezaji walishikilia mpango wao na kufanya vizuri.

"Wakati baada ya kusawazisha mchezo ulikuwa wakati wetu bora zaidi kwenye mechi."



## Maddison azigonganisha Utd, Spurs

**LONDON,** England

KLABU ya Leicester City itamuuza James Maddison msimu huu wa majira ya joto bila kujali jinsi mbio zao za kubakia Ligi Kuu ya England zinavyozidi, huku Manchester United na Tottenham Hotspur zikimwania.

Kwa mujibu wa Gazeti la Telegraph, Leicester itakubali ofa ya pauni milioni 45 kwa mchezaji huyo ili kusaidia kusawazisha vitabu vya klabu baada ya mwaka mgumu wa kifedha.

Kiungo huyo wa kati wa England mwenye umri wa miaka 26, amebakiza mwaka mmoja tu kukamilisha mkataba wake wa sasa pale kwenye Uwanja wa King Power na anatakiwa na klabu nyingi ukiacha Man United na Spurs, kwani Newcastle United nayo inatajwa kumwania.

Tangu ajiunge na Leicester mwaka 2018, mzaliwa huyo wa Coventry amejidhihirisha kuwa mmoja wa wachezaji muhimu kwenye Ligi Kuu - akiongeza mchango wa kuvutia wa mabao 20 ya moja kwa moja msimu uliopita.

Na licha ya matatizo ya majeraha na timu yake kupata matokeo, Maddison bado ameweza kufunga mabao tisa na kutoa pasi saba za mabao katika mechi 25 za Ligi Kuu msimu huu.

HABARI MICHEZO

75,029/-

# ABSA YAMWAGA MAMILIONI MBIO ZA DAR CITY MARATHON

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Watanzania wakishauriwa kulinda afya zao kwa kufanya mazoezi mbalimbali ya viungo kwa kuwa afya ni mtaji muhimu katika shughuli za uzalishaji mali, Benki ya Absa Tanzania, imetoa kiasi cha Sh. milioni 45 kwa ajili ya kudhamini mbio za Dar City Marathon zinazotarajiwa kufanyika jijini Dar es Salaam Jumapili wiki hii.

Ushauri huo umetolewa jijini Dar es Salaam jana na Mkuu wa Masoko na Mawasiliano wa Benki ya Absa Tanzania, Aron Luhanga, wakati akizungumzia udhamini wa Absa katika mbio za kilomita 21 zitakazojulikana kama Absa Dar City Marathon.

Luhanga alisema Benki ya Absa kwa kutambua kuwa afya ni mtaji mkubwa sana kwa wafanyakazi, wateja na kwa Watanzania kwa ujumla na kwamba bila kuwa na afya njema shughuli za kiuchumi haziwezi kwenda kadri zinavyotakiwa, benki yao imekubali kutoa udhamini wa mbio hizo wenye jumla ya Sh. milioni 45.

"Kama Absa tunajisikia furaha sana kuungana na waandaaji wa Dar City Marathon tukiwa wadhanini wakuu wa mbio hizi tukitoa udhamini wa kiasi cha Sh. milioni 45, zikiwa na lengo la kuisaidia jamii kupambana na magonjwa yasiyo ambukiza.

"Baada ya mbio hizi, tutaungana na Runners Club kwenda katika Hospitali ya Mnazi Mmoja ili kukabidhi vifaa vitakavyopatikana kupitia mbio hizi ili kusaidia magonjwa yasiyoambukiza," alisema Luhanga.

Mkuu wa Kitengo cha Habari wa Klabu ya The Runners, waandaaji wa mbio hizo, Godfrey Mwangungulu, alitoa shukurani kwa Absa pamoja na wadhanini wengine kwa kudhamini mbio hizo ambazo zaidi ya watu 3,000 watashiriki akisema pamoja mambo mengine zitasaidia kutangaza vivutio vya utalii vya Jiji la Dar es Salaam kwani zitapita katika mitaa mashuhuri ya jiji hilo.

Mbio za Absa Dar City Marathon zitajumuisha mbio za kilomita 21, mbio za kilomita 10 na mbio za kujifurahisha za kilomita 5 ambazo zawadi mbalimbali zitatolewa zikiwamo pesa tasilimu kwa mshindi wa kwanza hadi wa 10 kwa wanawake na wanaume.



Kutoka kulia ni Mkuu wa Kitengo cha Masoko na Mawasiliano cha Benki ya Absa Tanzania, Aron Luhanga, Mkuu wa Kitengo cha Habari wa Klabu ya The Runners, Godfrey Mwangungulu, Meneja Masoko na Mauzo wa Kampuni wa Bima ya Alliance Life Assurance, Jawa Masomo, Meneja Masoko wa Britam Insurance, Leoncia Makobo na Katibu wa The Runners, Scola Kisanga, wakionyesha fulana zitakazovaliwa siku ya mbio za Absa Dar City Marathon zinazotarajiwa kufanyika mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam. **MPIGAPICHA WETU**

## Robertinho aahidi furaha Simba leo

INATOKA UK. 24

alisema kocha huyo.

Kocha Mkuu wa Namungo, Denis Kitambi, amekiri kuwa mechi itakuwa ngumu kutokana na ubora wa Simba, lakini na wao wamejipanga kuhakikisha wanakabiliana nayo.

"Tunatambua kuwa tunacheza na timu ambayo ipo kwenye ubora wake, katika michuano ya kimataifa tumeiona, lakini kwenye ligi ipo nafasi ya pili na imekuwa inafanya vema, kwa hiyo na sisi ni lazima tuwe kwenye ubora pia. Mpaka sasa tumejiandaa vizuri, ila changamoto tuliyonayo ni kwamba kwa siku za karibuni tumekuwa hatuko vizuri kwenye safu yetu ya ulinzi na hicho ndicho kwa kiasi kikubwa tumekifanyia kazi," alisema kocha huyo.

## *Marumo: Yawaita Simba*

INATOKA UKURASA 24

nusu fainali.

Aliyewahi kuwa Kocha Mkuu wa Simba, Dylan Kerr, amefunguka ana uhakika mkubwa wa kupata matokeo katika mchezo wa kwanza wa nusu fainali wa Kombe Shirikisho Afrika dhidi ya Yanga.

Akizungumza na Nipashe jana kwa njia ya simu kuelekea mchezo huo, Kerr alisema anakuja nchini kwa kazi ya kuhakikisha wanapata ushindi na akiamini atapa sapoti kubwa kutoka kwa Simba katika mchezo huo wa kwanza kabla ya mchezo wa marudiano utakaopigwa Afrika Kusini Mei 17, mwaka huu.

Alisema hawana presha ya mchezo dhidi ya Yanga kwa sababu anawajua vizuri na tayari wameanza kuwafuatilia kupitia watu wao na mechi walizocheza hivi karibuni kuona ubora na madhaifu yao.

"Si mgeni na Tanzania, tayari nimewahi kufanya kazi na Simba ambao ni familia yangu, malengo yetu kama timu ni kuona tunashinda kwa kupita kila hatua ya michuano hii mikubwa Afrika.

"Naamini matokeo ya ushindi tunayotarajia kuyapata katika mchezo wa kwanza Tanzania, yatachagizwa na Simba pamoja mashabiki wao kwa sababu itakuwa ni furaha kubwa kuona tumewafunga wapinzani wao licha ya kwamba tunapita katika kipindi kigumu katika ligi ya nyumbani kwa kupambania kubakia Ligi Kuu, lakini hatuwezi kusitisha malengo," alisema Kerr.


SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 06/05/23 | 17:00 | Wolverhampton Wanderers vs Aston Villa | 2.85 | 3.15 | 2.36 |
| 02. 06/05/23 | 18:00 | OGC Nice vs Stade Rennes | 2.65 | 3.15 | 2.55 |
| 03. 06/05/23 | 19:00 | AS Roma vs Inter Milano | 2.60 | 3.05 | 2.65 |
| 04. 06/05/23 | 21:45 | US Cremonese vs Spezia Calcio | 2.20 | 3.25 | 3.05 |
| 05. 06/05/23 | 22:00 | RC Lens vs Olympique Marseille | 2.23 | 3.40 | 2.90 |
| 06. 07/05/23 | 00:00 | CA Belgrano vs Atletico Tucuman | 2.20 | 2.95 | 2.90 |
| 07. 07/05/23 | 02:30 | Charlotte FC vs New York City FC | 2.41 | 3.05 | 2.55 |
| 08. 07/05/23 | 02:30 | San Jose Earthquakes vs Los Angeles FC | 2.60 | 3.20 | 2.26 |
| 09. 07/05/23 | 02:30 | Inter Miami CF vs Atlanta United FC | 2.36 | 3.15 | 2.50 |
| 10. 07/05/23 | 13:30 | Umraniyespor vs Sivasspor | 2.75 | 3.15 | 2.16 |
| 11. 07/05/23 | 13:30 | Atalanta BC vs Juventus Turin | 2.31 | 3.25 | 2.85 |
| 12. 07/05/23 | 16:00 | FC Nantes vs Strasbourg Alsace | 2.50 | 3.30 | 2.60 |
| 13. 07/05/23 | 16:00 | AJ Auxerre vs Clermont Foot 63 | 2.25 | 3.20 | 3.00 |
| 14. 07/05/23 | 16:00 | FC Lorient vs Stade Brest 29 | 2.22 | 3.40 | 2.90 |
| 15. 07/05/23 | 17:30 | Maritimo Madeira vs Rio Ave FC | 2.43 | 3.00 | 2.90 |
| 16. 07/05/23 | 18:30 | Newcastle United vs Arsenal FC | 2.40 | 3.40 | 2.65 |
| 17. 07/05/23 | 20:00 | Vitoria SC Guimaraes vs FC Vizela | 2.31 | 3.10 | 3.00 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATANO - 03/05/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 11:00 | 1325 | Tokyo Verdy vs Jubilo Iwata | 2.33 | 3.07 | 2.82 |
| 13:00 | 1075 | Shakhtar Donetsk vs FC Minaj | 1.16 | 5.92 | 12.25 |
| 13:00 | 2908 | SC Dnipro 1 vs FC Metalist Kharkiv | 1.21 | 5.55 | 9.46 |
| 13:00 | 4206 | Gyeongnam vs Seoul E Land | 2.06 | 3.23 | 3.18 |
| 13:00 | 5165 | Yokohama vs Niigata Albirex | 3.07 | 3.33 | 2.07 |
| 15:00 | 4502 | Zorya Lugansk vs Veres Rivne | 1.43 | 4.07 | 5.98 |
| 16:00 | 3279 | Orlando Pirates vs Bloemfontein Celtic | 1.64 | 3.50 | 5.12 |
| 17:00 | 5412 | Ural Yekaterinburg vs CSKA Moscow | 3.46 | 3.15 | 2.03 |
| 18:00 | 2739 | Ararat Armenia vs Ararat Yerevan | 1.33 | 4.56 | 7.88 |
| 18:00 | 4020 | Ethiopia Electricity vs Ethiopian Medhin | 3.41 | 3.20 | 2.02 |
| 18:15 | 1573 | Maritzburg Utd vs Marumo Gallants FC | 2.53 | 2.88 | 2.88 |
| 18:15 | 4572 | Sekhukhune United vs TS Galaxy FC | 2.12 | 2.89 | 3.67 |
| 18:30 | 1607 | Hifk vs TPS Turku | 2.63 | 3.19 | 2.40 |
| 19:00 | 1416 | Atalanta vs Spezia | 1.35 | 4.71 | 7.22 |
| 19:00 | 1431 | Salernitana vs Fiorentina | 4.29 | 3.64 | 1.72 |
| 19:00 | 1650 | Sampdoria vs Torino | 4.08 | 3.34 | 1.83 |
| 19:00 | 1695 | Bodo Glimt vs Odd Ballklubb | 1.28 | 5.45 | 8.38 |
| 19:00 | 1856 | Juventus vs Lecce | 1.60 | 3.51 | 5.50 |
| 19:00 | 5574 | Rosenborg vs Brann | 2.94 | 3.36 | 2.24 |
| 20:00 | 2912 | Kalmar vs Sirius FK | 1.77 | 3.34 | 4.06 |
| 20:00 | 3480 | Elfsborg vs Halmstads BK | 1.42 | 4.21 | 5.96 |
| 20:00 | 3715 | Sparta Prague vs Slavia Prague | 2.42 | 3.32 | 2.59 |
| 20:00 | 4804 | BK Hacken vs Djurgardens IF | 1.85 | 3.44 | 3.59 |
| 20:00 | 4943 | Mjallby vs AIK Football | 2.67 | 2.93 | 2.54 |
| 20:30 | 2906 | Cape Town City vs Golden Arrows | 2.09 | 3.14 | 3.40 |
| 20:30 | 3315 | Valencia vs Villarreal | 2.79 | 3.29 | 2.33 |
| 20:30 | 4521 | Amazulu vs Mamelodi Sundowns | 4.50 | 3.46 | 1.73 |
| 20:30 | 5178 | Sivasspor vs Fenerbahce | 3.99 | 3.58 | 1.75 |
| 20:30 | 5782 | Beitar Jerusalem vs Maccabi Tel Aviv | 10.37 | 5.18 | 1.23 |
| 20:30 | 5784 | Richards Bay FC vs Chippa Utd | 2.14 | 3.02 | 3.44 |
| 21:00 | 1286 | KA Akureyri vs Hafnarfjordur | 1.98 | 3.42 | 3.31 |
| 21:00 | 1371 | Umm-Salal SC vs Al-Shamal | 2.01 | 3.34 | 3.19 |
| 21:00 | 3107 | AL Markhiya vs Al-Sailiya SC | 2.22 | 3.44 | 2.72 |
| 21:15 | 4946 | ND Gorica vs NK Celje | 3.55 | 3.24 | 1.92 |
| 21:30 | 2341 | Al Shabab Riyadh vs Al Fateh (KSA) | 1.59 | 4.20 | 4.89 |
| 21:30 | 3345 | Al Wehda vs Dhamk | 2.20 | 3.35 | 3.14 |
| 21:45 | 1855 | Crewe vs Bradford City | 4.25 | 3.61 | 1.70 |
| 21:45 | 2383 | Woking vs Bromley | 1.95 | 3.20 | 3.83 |
| 21:45 | 4904 | Burton vs Cambridge Utd | 3.07 | 3.27 | 2.23 |
| 21:45 | 5582 | Stuttgart vs Eintracht Frankfurt | 2.37 | 3.33 | 2.95 |
| 22:00 | 1010 | Liverpool vs Fulham | 1.28 | 5.27 | 8.36 |
| 22:00 | 1155 | AC Milan vs Cremonese | 1.29 | 4.89 | 9.18 |
| 22:00 | 1248 | Brest vs Nantes | 2.19 | 3.26 | 3.06 |
| 22:00 | 2526 | Monza vs Roma | 3.40 | 3.05 | 2.13 |
| 22:00 | 3029 | Verona vs Inter | 4.81 | 3.61 | 1.65 |
| 22:00 | 4441 | Manchester City vs West Ham | 1.23 | 5.59 | 9.92 |
| 22:00 | 5685 | Lazio vs Sassuolo | 1.63 | 3.80 | 4.70 |
| 22:15 | 4517 | KR Reykjavik vs HK Kopavogs | 1.65 | 3.95 | 4.15 |
| 23:00 | 2783 | Getafe vs Celta Vigo | 2.44 | 2.89 | 2.99 |
| 23:00 | 3692 | Atletico Madrid vs Cadiz CF | 1.26 | 5.20 | 9.60 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo

Jumatano Mei 3, 2023

Nipashe



City kila mechi ni fainali-Alvarez UKURASA 22

# Kocha Marumo awaita Simba kuwabeba Vs Yanga CAF

●●● Ni Kerr aliyewahi kuwanoa Wekundu wa Msimbazi, asema wataichapa kwa Mkapa...

**Na Saada Akida**

WAKATI Shirikisho la Soka nchini (TFF), likiikubalia Klabu ya Yanga ombi lao la kusogezwa mbele tarehe ya mechi ya nusu fainali Kombe la FA dhidi ya Singida Big Stars, ili kupata muda wa kujiandaa na mchezo wao wa mkondo wa kwanza wa nusu fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Marumo Gallants FC ya Afrika Kusini, Kocha wa Wasauzi hao, Dylan Kerr, amesema "Simba watakuwa upande wetu na tutapata matokeo ugenini".

**Yanga itacheza na Singida Big Stars kesho Mei 4, katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayopigwa Uwanja wa Liti mjini Sindiga, na kabla ya TFF kuridhia ombi lao la kusogezwa mbele mchezo wao wa nusu fainali wa Kombe la FA dhidi ya 'Walima Alizeti' hao, ilikuwa washuke tena uwanjani hapo Jumapili wiki hii.**

Pia wawakilishi hao pekee wa Tanzania katika michuano ya kimataifa, watakuwa na kibarua kigumu Mei 10, mwaka huu cha kuendelea kuipeperusha vema bendera ya Tanzania katika mechi ya kwanza ya nusu fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Marumo Gallants FC itakayopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Awali, akizungumza na Nipashe jana kabla ya TFF kuridhia ombi lao, Rais wa Yanga, Injinia Hersi Said, alisema kulingana na ratiba ya mechi zao, imekuwa si rafiki kutokana kuwa na mechi tatu mfululizo kila baada ya siku tatu.

Alisema walikuwa wacheze mechi Mei 4 na 7, dhidi ya Singida Big Stars kwenye Ligi Kuu na Kombe la FA na michezo yote kuchezwa, Singida na baada ya mechi hizo walitakiwa kurejea Dar es Salaam kwa ajili ya maandalizi ya mechi ya nusu fainali ya CAF dhidi ya Marumo Gallants, Mei 10, mwaka huu hivyo waliandika barua kwa TFF kuomba kupangiwa tarehe nyingine.

"Tukisema tucheze mechi ya FA, Mei 7 na 8 turudi Dar es Salaam, tutakuwa na siku moja ya maandalizi ya mechi yetu dhidi ya Marumo Gallants kwa sababu ingewezekana kama kungekuwa na usafiri wa ndege kutoka Singida, basi tungecheza mchezo wetu huo na kurudi haraka siku hiyo ili kujiandaa na mchezo wa nusu fainali ya Afrika," alisema Hersi.

Hata hivyo, mapema jana hiyo hiyo TFF iliijibu Yanga kwa kuridhia ombi hilo baada ya kueleza: "TFF kwa kuzingatia maslahi mapana ya nchi, imekubali kusogeza mbele mchezo kati ya Singida BS na Yanga uliopagwa kuchezwa Mei 7, mwaka huu katika Uwanja wa Liti mpaka hapo utakapopangiwa tarehe nyingine."

Katika hatua nyingine, pia TFF imesogeza mbele mchezo wa nusu fainali kati ya Azam FC na Simba uliopangwa kuchezwa Jumamosi Aprili 6 na sasa utachezwa Jumapili Aprili 7, mwaka huu sababu ikiwa ni kuzipa timu hizo muda wa maandalizi zaidi.

Wakati hayo yakijiri kwa TFF kuridhia ombi la Yanga kupewa muda wa maandalizi, wapinzani wao, Marumo Gallants wemesema wanaamini watapata matokeo chanya katika mchezo huo wa

INAENDELEA UKURASA 23



ROBERTINHO

## Robertinho aahidi furaha Simba leo

**Adam Fungamwango na Shufaa Lyimo**

BAADA ya kutolewa kwenye hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa mikwaju ya penalti 4-3 dhidi ya Mabingwa Watetezi, Wydad Athletic Club ya Casablanca, Morocco, timu ya Simba leo inarejea kwenye mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara kucheza dhidi ya Namungo FC mchezo utakaopigwa Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa mkoani Lindi.

Kwa zaidi ya siku 15, Simba haijacheza mechi yoyote ya Ligi Kuu tangu ilipofanya hivyo Aprili 16, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, ilipocheza dhidi ya watani zao wa jadi, Yanga na kushinda mabao 2-0.

Hivyo, kwa mara ya kwanza baada ya siku hizo kupita, timu hiyo inashuka uwanjani ikiwa na kazi moja tu ya kuwaliwaza mashabiki wake kwa ushindi, huku ikijaribu kupunguza pengo la pointi ilizonazo dhidi ya timu ya Yanga inayoongoza ligi kwa pointi 68.

Iwapo ikishinda, itafikisha pointi 66, na itakuwa imebakisha pengo la pointi mbili ambalo linaweza kubaki lilivyo au kuongezeka wakati Yanga itakapoivaa Singida Big Stars kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara hapo kesho.

Kocha Mkuu wa Simba, Robertinho Oliveira, amesema pamoja na kutolewa kwenye michuano ya kimataifa wachezaji wake na benchi la ufundi hawajavunjika moyo na kwamba watapambana kadri ya uwezo wao kushinda na kuwafurahisha wanachama na mashabiki wao ambao wamekuwa wakiwapa nguvu na sapoti kila wanapokwenda, wanapofanya vizuri na hata wanapoanguka.

"Tuna mechi mbili dhidi ya Namungo [leo] na Azam [Jumapili], tunakwenda kuzicheza zote kwa ufanisi mkubwa na kuwafurahisha wanachama na mashabiki wetu ili kusahau yaliyopita, tutacheza mechi kama zingine zote zilizopita,"

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >